SportPesa
TZS. 1,255,316,060
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 3

**CCM yajitosa suala ruzuku ya pembejeo**




UKURASA 11

Nipashe
Jumamosi Mei 14, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580945
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Sakata kina Mdee bado kizungumkuti

**KATIBA** ya nchi yaweka wazi uamuzi wa kuchukuliwa dhidi yao... *Endelea Ukurasa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan akionyesha ripoti ya miaka 10 ya Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), baada ya kuizindua katika maadhimisho ya miaka 10 ya mtandao huo, Dar es Salaam jana. Wengine ni Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro (kulia), Mwenyekiti wa THRDC, Jaji Mstaafu Joaquine De Mello (wa pili kushoto) na Mratibu wa Mtandao huo, Onesmo Olengurumwa. **PICHA: IKULU**

## Rais Samia awakosha watetezi haki, asema hakuna mapambano

UKURASA 2

## NGO 4,900 katika hatari kufutiwa usajili

UKURASA 3

MICHEZO **MWISHO WA MORRISON SIMBA?** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Sakata kina Mdee bado kizungumkuti

**Na Waandishi Wetu**

HATIMA ya wabunge 19 wa viti maalum waliovuliwa uanachama na vikao vya juu vya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) bado ni kizungumkuti kutokana na uongozi wa Bunge kutochukua hatua dhidi yao.

Baadhi ya wabunge hao ambao Baraza Kuu la CHADEMA lilitangaza usiku wa kuamkia juzi kuunga mkono uamuzi wa Kamati Kuu wa kuwavua uanachama, jana walihudhuria kikao cha Bunge la Bajeti jijini Dodoma.

Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alipoulizwa na Nipashe kuhusu barua yao kwa uongozi wa Bunge dhidi ya wabunge hao, alidai tayari imeshafika rasmi mezani kwa Spika.

Alidai kuwa waliwasilisha barua hiyo kwa Spika jana asubuhi kumjulisha kuhusu uamuzi wa Baraza Kuu kuwa limeridhia wabunge hao 19 kufutwa uanachama wa CHADEMA.

"Kwa hiyo, ni wajibu wa Spika kuchukua hatua, wao kwenda bungeni siyo tatizo kwa sababu bado Spika hajachukua hatua, tunasubiri Spika atoe kauli," alisema.

**KUTAMBUA UCHAGUZI**

Alipoulizwa na Nipashe kama CHADEMA itapeleka majina mapya ya wabunge wa viti maalum ilhali ilishatangaza haikutambua Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Mrema alisema mpaka sasa suala hilo halijazungumzwa na litategemea hatua ambazo Spika atazichukua dhidi ya wabunge hao 19 wanaoongozwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA).

"Kamati Kuu ikiamua kuteua au isipoteua ni wajibu wake. Kwa sasa hakuna kauli kwa sababu Kamati Kuu haijakaa na kujadili jambo hili," alisema.

**WATINGA BUNGENI**

Licha ya uamuzi wa kuvuliwa uanachama ulioridhiwa na Baraza Kuu juzi, baadhi ya wabunge hao jana waliingia bungeni majira ya saa tatu asubuhi na kushiriki kikao cha chombo hicho.

Wabunge ambao Nipashe iliwashuhudia bungeni jana kutoka kundi hilo la wabunge 19 waliofutwa uanachama: Salome Makamba, Esther Matiko, Tunza Malapo, Jesca Kishoa, Anatropia Theonest, Asya Mohamed, Stella Fiao.

Wakiwa kwenye shughuli za Bunge kipindi cha 'Maswali', baadhi ya wabunge hao walipewa nafasi ya kuuliza maswali ambayo yalijibiwa na mawaziri husika. Waliopata nafasi ya kuuliza swali ni Salome, Tunza na Asya.

**MWENYEKITI MAADILI**

Nipashe ilizungumza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Kinga, Maadili na Madaraka ya Bunge, Emmanuel Mwakasaka, kwa lengo la kupata maoni kuhusu kurejea kwa wabunge hao bungeni licha ya kufutwa uanachama wa CHADEMA.

Mwakasaka alisema: "Msemaji Mkuu wa suala hilo ni Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackon, yeye ndiye atatuambia kama mkuu wa mhimili huu kuna nini kinaendelea.

"Kwa sababu yale yaliyotokea CHADEMA hayaingii moja kwa moja kwenye Bunge, sisi hatufahamu kama Spika ameshapokea taarifa."

Mwakasaka ambaye pia ni Mbunge wa Tabora Mjini, alisema amewaona bungeni wabunge hao na bado anawatambua kuwa ni wabunge.

"Wenzetu tumewaona leo (jana) bungeni na bado tunawatambua kama wabunge wenzetu, ndiyo maana leo wapo bungeni. Sasa katika hatua hii sisi tunasubiri taarifa ya mkuu wetu wa mhimili atatueleza nini. Lakini haya matangazo mengine tunaendelea kuyasubiri kutoka kwa Spika," alisema Mwakasaka.

Alisema kama kuna barua imeandikwa, itapelekwa kwa mhusika ambaye ni Spika wa Bunge au Katibu wa Bunge, akifafanua: "Kuna wakati barua wanaielekezea kwa Spika wa Bunge mwenyewe, sasa ikishafika nini kinakuja baada ya hapo? Spika mwenyewe atatujulisha sisi wenyeviti wa kamati, lakini hadi sasa tunavyozungumza na ninyi hatujapokea taarifa yoyote kutoka kwa Spika."

**KATIBA INASEMAJE?**

Kifungu cha 1(e) cha Ibara ya 71 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, kinaelekeza hatua za kuchukuliwa dhidi ya mbunge aliyepoteza uanachama wa chama cha siasa.

Inatamkwa katika kifungu hicho kuwa: "Mbunge atakoma kuwa mbunge na ataacha kiti chake katika Bunge ikiwa mbunge huyo ataacha kuwa mwanachama wa chama alichokuwamo wakati alipochaguliwa au alipoteuliwa kuwa mbunge."

■**Imeandikwa na Gwamaka Alipipi (DODOMA na Romana Mallya (DAR)**



Baadhi ya Wabunge wa Viti Maalum wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), waliofutwa uanachama na Baraza Kuu la Chama hicho, wakiingia Bungeni, jijini Dodoma jana, kuhudhuria kikao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Samia awakosha watetezi wa haki

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka watetezi wa haki za binadamu kuacha mapambano na serikali na badala yake waungane na kufanya kazi kwa pamoja.

Vilevile, amewataka kuacha kutetea haki za wanasiasa tu na badala yake wageukie makundi mengine yanayohitaji watetezi kama watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili na wanaopoteza maisha kwa ajali za barabarani, pia kutoa elimu kwa jamii kuhusu haki na wajibu hasa kwa makundi hatarishi kama 'panya road'.

Rais Samia aliagiza hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya miaka 10 ya Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC).

Alisema wanatakiwa kukaa mezani na kufanya kazi kwa sababu katika uongozi wake hakuna mapambano.

"Nikisikia watu wakija na ule uanaharakati, siwakatazi lakini uanaharakati 'positive' (chanya) ndiyo unajenga, kama mna jambo njooni tuzungumze, kuna vyombo vya ulinzi na usalama kaeni navyo mzungumze," alisema Rais Samia.

Aliwataka kufanya harakati wa haki za binadamu kwa mazingira ya Kitanzania na kuacha kupambana na serikali kusiko na tija.

"Hasa ikizingatiwa nchi ina mama, mama hapambani, njooni tukae tuzungumze," alisisitiza Rais Samia na kusema Watanzania wanatakiwa kukaa pamoja na kuisuka upya nchi na kuwa na umoja na mshikamano.

"Sasa kama kuna sera ya nchi, unapambana na nani, unapambana na mama? Ukipambana na mama kwa Mungu hakuna baraka," Rais Samia alisema.

Aliongeza kuwa nchi ina sheria na taratibu za Kitanzania, hivyo wakati wanafanya utetezi wanatakiwa kuzingatia hilo.

Alisema watetezi wakijikita kutetea haki za binadamu, wafanyakazi na wakulima, haki zitarejea na mabadiliko yatafanyika, pia wakosoe pale serikali inapokosea kwa kutumia lugha nzuri.

"Mkitumia lugha mbaya haitakuwa na maana kupatiwa majibu mazuri, ni 'approuch' (mbinu) ndiyo inayomata, twende na 'approach' (mbinu) nzuri ya kujenga Taifa," alisema.

Aliwakumbusha hakuna atakayekusaidia kujenga Taifa isipokuwa Watanzania wenyewe kwa kukaa pamoja na kujenga nchi.

Rais Samia pia aliwataka watetezi wa haki za binadamu kuelimisha wananchi kujua kuhusu katiba ili wanapodai Katiba Mpya wajue na haki zao ni zipi katika katiba hiyo wanayodai.

"Ndiyo maana nimesema tuelimishane kuhusu haki na wajibu ili akitokea wa kumkorofisha mwenzie anaposhughulikiwa isionekane ameonewa, bali amefanyiwa hivyo kwa kuvunja haki ya wenzake," alisema Rais Ramia.

Kuhusu watetezi wa haki za binadamu, Rais Samia alisema kwa muda mrefu walikuwa wamejielekeza kwenye haki za wanasiasa kuliko haki za watoto.

Alisema kuna watoto wanabakwa na kufanyiwa ulawiti lakini hakuna wanaowatetea, pia kuna panya road lakini wanaozungumza hakuna watetezi wa haki za binadamu wailozungumza kuhusu vijana hao kutotimiza wajibu wao kwa kuvunja sheria na hakuna anayezungumza nao.

Alisema kuna ajali za barabarani lakini hakuna anayezungumzia kuhusu watu kupoteza maisha zaidi ya asasi inayojihusisha na ajali za aina hiyo.

Kuhusu malalamiko ya sheria yaliyotolewa na watetezi hao, aliwataka kupataja wapi inapowabana, akisema: "Ninajua moja ya eneo ni uwazi wa fedha mnazopokea kutoka nje na namna mnavyozitumia."

Alisema wameamua kufanya hivyo kulingana na matakwa ya dunia kuwa, kuwe na taarifa za fedha zinazoingia nchini na matumizi yake.

Alisema ripoti za wafadhili zimekuwa zikitaja fedha nyingi zinazoingia nchini, lakini serikali inakuwa haifahamu chochote kuhusu fedha hizo.

Rais Samia alisema wanataka wafahamu wanachofanya nchini kupitia fedha za miradi wanazopokea kutoka nchini.

Awali, Mratibu Kitaifa wa THRDC, Onesmo Ole Ngurumwa, aliomba serikali kuwasaidia eneo la kujenga jengo la Watetezi, ambalo litatumiwa na watetezi wa haki za binadamu wa ndani na nje ya nchi.

Pia aliiomba serikali kuwa na sheria na sera za kuwatambua watetezi wa haki za binadamu nchini ili kufanya kazi zao kwa uhuru na amani.

Alisema miaka ya nyuma walipitia vikwazo mbalimbali ikiwamo kubambikwa kesi, kuonekana wapinzani na kufungiwa akaunti zao.

Aliishukuru serikali kwa kukubali mapendekezo makubwa ya kimataifa yakiwamo ya watetezi wa haki za binadamu na haki za binadamu.

Katika maadhimisho hayo, Rais Samia alizindua ripoti inayozungumzia hali ya watetezi wa haki za binadamu na asasi za kiraia nchini kwa miaka 10.

Wakili wa THRDC, Leopod Mosha, alisema hali ya watetezi wa haki za binadamu nchini imeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka licha ya uwapo wa vikwazo mbalimbali.

Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright, aliiomba THRDC kuendelea kufanya kazi ya utetezi wa haki za binadamu na kusimamia upatikanaji wa haki miongoni mwa jamii.

Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shahibu, aliwapongeza THRDC katika kuhakikisha wanasimama na kutetea haki za wanaharakati waliokuwa wakikamatwa katika nyakati mbalimbali.

Alisema wakati wakuadhimisha miaka 10 ni muhimu kupatikana kwa Katiba Mpya ili kujenga misingi ya ufanyaji kazi za watetezi wa haki za binadamu.

■**Imeandikwa na Mary Geofrey na Beatrice Shayo**

# CCM sasa yajitosa ruzuku ya pembejeo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeziagiza Wizara ya Fedha na Mipango na ya Kilimo kuharakisha uandaaji wa muundo wa namna ya kutoa ruzuku ya mbolea ili kuwapunguzia mzigo wa gharama wakulima katika msimu ujao wa kilimo.

Uandaaji wa utaratibu huo ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan alilolitoa hivi karibuni jijini hapa alipokuwa akigawa vitendea kazi kwa maofisa ugani nchini.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alitoa agizo hilo jana alipotembelea ujenzi wa kiwanda cha uzalishaji mbolea ya asili cha Itracom, kinachojengwa na mwekezaji kutoka Burundi ambacho kinagharimu zaidi ya Sh. Bilioni 480.

Alisema wizara hizo zinatakiwa hivi karibuni ziweke wazi namna zitakavyotekeleza utaratibu huo.

"Kwenye mkutano wa maofisa ugani, Rais alitoa agizo kwa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha kukaa pamoja kuweka utaratibu wa kuhakikisha inatengeneza uhakika wa upatikanaji wa mbolea kwa bei nzuri isiyo mzigo kwa mkulima," alisema.

Alisema mbolea inayohitajika nchini ni tani 700,000 na kiwanda hicho kitazalisha tani 600,000 kwa mwaka baada ya kukamilika na kwa awamu ya kwanza uzalishaji utaanza kati ya Juni na Julai, mwaka huu, ambapo zitazalishwa tani 200,000.

"Kwa hiyo kwa mwaka ujao tutakuwa na upungufu wa tani 500,000 ambazo unahitajika mpango ili mkulima apate mbolea, kwa hiyo tumeona hili jambo lisipite hivi tuhakikishe kunakuwepo na uhakika wa mbolea na uhakika wa utekelezaji wa maagizo ya Rais ya kuondoa changamoto ya mbolea katika msimu ujao,"alisema.

Kuhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Chongolo alisema lazima sasa ifanye kazi kibiashara, kiushindani kwa kusimamia wanakuwa daraja la kuangalia bei ya mbolea na upatikanaji rahisi wa bidhaa ya mbolea bila kufanya hivyo haitakuwapo haja ya uwapo wao.

Aliagiza ruzuku hiyo ilenge kukuza tija ya uzalishaji wa mbolea ya ndani ya nchi ili kulinda wawekezaji na kuhamasisha wengine kuja kuwekeza.

"Tusiweke ruzuku halafu mbolea tukaenda kuagiza nje. Kwanza kiwe ni kile kinachopatikana ndani ya nchi halafu kinachobakia ndipo mfikirie nje ya nchi ili kulinda wawekezaji wa ndani na kuhimiza wengi kuwekeza kwenye uzalishaji wa mbolea," alisema.

Aliwahimiza wawekezaji wakubwa kuwekeza Dodoma kutokana na kuwa na eneo kubwa la uwekezaji. Naye msimamizi wa ujenzi wa kiwanda hicho, Msafiri Dieudonne, alisema kiwanda hicho kimekamilika kwa asilimia 80 na Mwezi Julai mwaka huu kitaanza uzalishaji kwa awamu ya kwanza.

"Bei ya mbolea itakuwa chini ili kupunguza gharama na wanaofanya hesabu wameshaanza kufanya na mwisho wa mwezi Agosti watatoa majibu,"alisema.

Awali, Meneja kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Abubakar Ndwata, alisema kiwanda hicho kitatoa ajira za moja kwa moja kwa watu 3,000 na kuwataka watanzania kuchangamkia fursa za uwapo wa kiwanda hicho.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alimpongeza mwekezaji wa kiwanda hicho ambaye ni raia wa Burundi kwa kuwekeza mkoani Dodoma jambo ambalo alisema litaondoa dhana iliyopo kwa watu kuwa Mkoa huo ni wa shughuli za serikali pekee.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Prof. Yunus Mgaya, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam, jana, kuhusu kongamano la 31 la Kisayansi litakalo zinduliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Mei 17, mwaka huu katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Julias Nyerere. Kushoto ni Mkurugenzi Mratibu wa Taarifa na Mawasiliano ya Kitafiti, Dk. Ndekya Oriyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NGO 4,900 hatarini kufutiwa usajili

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

ZAIDI ya mashirika 4,900 yasiyo ya kiserikali (NGO) yako hatarini kufutiwa usajili kutokana na kukiuka sheria na taratibu zinazoyaongoza.

Kutokana na kukiuka huko, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju, ameyataka kujieleza kwa nini yasifutiwe usajili kwa kitendo hicho.

Mpanju alitoa agizo hilo jana alipokutana na NGO za Mkoa wa Iringa katika ziara yake ya siku mbili mkoani hapa yenye lengo la kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya wizara.

Mpanju alisema mashirika hayo yameshindwa kutekeleza matakwa ya kisheria ikiwamo kuwasilisha taarifa zao kwa ajili ya uhakiki, lakini tangu uhakiki huo uanze mwaka jana, yameshindwa kufanya hivyo.

"Hadi kazi hiyo ya uhakiki inakamilika Machi, mwaka huu, ni mashirika 4864 kati ya 12,884 yamehakikiwa na mashirika 7,533 ndiyo yako hai. Sasa niwaombe NaCONGO

(Baraza na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali) hakikisheni yale mashirika ambayo hayakuhakikiwa kwa kipindi cha mwaka mmoja, yaeleze sababu kwa nini yasifutiwe ndani ya mwezi mmoja. Hapa Iringa ni mashirika 79 kati ya 170," alisema.

Naibu Katibu Mkuu alisema serikali inatambua mchango mkubwa unaofanywa na mashirika hayo katika kutekeleza shughuli na huduma mbalimbali kama elimu, afya maji na huduma mtambuka ikiwamo kusaidia kupambana na ukatili na kuchangia amani na utulivu nchini.

Mpanju alisisitiza kuwa serikali inafanya uhakiki ili kuhakikisha uratibu wa mashirika unakuwa na ufanisi na pia ni matakwa ya sheria ya nchi. Aliongeza kuwa hakuna budi kuratibu shughuli zinazofanywa na NGO kwa kuwa kazi zinazofanywa ni kubwa.

Katika hatua nyingine, Mpanju aliwaagiza wasajili wasaidizi wa NGO kuwapitisha wadau kwenye miongozo mbalimbali ya NGO ambayo inaeleza serikali na sekta mbalimbali zinavyoshirikiana ili kufanya kazi kwa ufanisi.

"Nyie wasajili wasaidizi ndiyo wasimamizi wa sekta hii kwa niaba ya wizara, hivyo mnapokuwa na majukwaa kama haya, wapitisheni, hakikisheni mwongozo unasambazwa kwani ndio unatoa utaratibu mzuri wa namna ya kushirikiana bila migongano," alisisitiza.

Mmoja wa wadau wa NGO, Lediana Mng'ong'o, kutoka shirika la TAHEA alishauri mashirika ambayo yalikuwa yamesajiliwa kabla ya usajili wao kuhamishiwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, yafutiwe na yasajiliwe upya kutokana na changamoto ya kulipa malimbikizo ya nyuma.

Naye Mtunza Hazina wa NaCONGO, John Kiteme, alisema baraza hilo linafanya kazi kwa kushirikiana na serikali kuhakikisha NGO zinafanya kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni, ikiwemo mchakato wa kusajili na kufuta mashirika.

Awali, Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Iringa, Saida Mgeni, alisema mashirika yaliyosajiliwa mkoani hapa ni 170 lakini yaliyo hai ni 91 na 79 yanasuasua kutokana na kutotekeleza malengo yao kwa mujibu wa usajili wao na kutokidhi matakwa ya sheria ikiwamo kutolipa ada na kutowasilisha taariza zao za utekelezaji.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**

**Wilaya ya Morogoro**

**Mkoa Wa Morogoro**

**Usimamizi wa Mirathi Na...29...2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MUSTAFA ABDALLAH SUGURU WA KIHONDA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA JANETH THOMAS MZIGO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 16 Mwezi 05 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa Tarehe 09 Mwezi 05 Mwaka 2022.

Imetolewa leo tarehe 09 Mwezi 05 Mwaka 2022

HAKIMU



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe:@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P. 2888,**
**DODOMA,**
**14 - 05 - 2022**

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatatu tarehe 16 – 05 – 2022 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Rufiji**, gari yenye namba za usajili: **T 296 CZS/ T 887 DJB**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 25.00** |
| **Upana** | - | **mita 4.20** |
| **Kimo** | - | **mita 4.80** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam Port hadi Rufiji Kupitia Pwani, mpaka Rufiji** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

*216856402*

# MATANGAZO

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**AGNESS SOSPETER** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0001** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ASIA SADICK** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0002** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**CAROLINE MSEMWA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0003** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**CARREN SHIRIMA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0004** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**EASTHER MAGOTI** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0008** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP




**EDINE MWAUZI** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0005** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**EDITHA MWAKAGATE** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0006** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ELIZABETH GODFREY** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0007** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**FATUMA MSUMENO** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0009** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**GLADNESS KIWELU** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0010** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**HADIJA MTONDA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0011** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**HANIFA MWANYIKA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0012** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**HOLINESS MAKISHA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0013** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**HONORATHA WISO** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0014** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**KABWE HAMIM** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0016** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**KURUTHUM OMARY** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0017** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**LINAH CHABAI** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0018** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**LISA CHABAI** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0019** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**MARIA MPONDA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0020** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**MARION MOSHI** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0021** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

# MATANGAZO

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**NEEMA ABDALLAH** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0022** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**NURU KAMBI** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0023** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**PERUS MGETA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0024 i**liyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ROSA MAKERE** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0026** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**SABRA LIWOWA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0027** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**SALOME LABAN** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0028** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER m**waka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**SAMRA ZUBERI** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0029** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**VANESA MOSHA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0030** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**WINIFRIDA THOMAS** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0031** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**WITNESS VICENT** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0032** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ZAINAB MDOE** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4446/0033** iliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUTHER** mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PWA/MAP/RB/184680/2022.**

**Magistrates Court( Approved Forms For the Primary Court) GN. NO 943(Contd.)**

**FOMU MADAI -3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**

**Kituo cha Marangu Mkoa Kilimanjaro**
**Shauri la Ndoa Na 02, 2022**

**Jina la Mdai GODBLESS HUDSON CHAO**

**Jina la Mdaiwa MAGRETH JOHN SHIRIMA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: Fred Magreth John Shirima MAMSERA ROMBO**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yake /yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai )

**MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 12 mwezi 05 mwaka 2022 saa 03:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 09 mwezi 05 Mwaka 2022

**JUDICIARY SUMMONS TO DEPENDANT**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI; MDAIWA**
**MCA/63**

**MAHAKAMA YA MWANZO YA MWANJELWA WILAYA YA MBEYA**

**SHAURI YA MADAI YA 32.................................2019**

**MDAI; MKURUGENZI WA SHULE WA SHULE SAKAMBONA SEC SCHOOL**

**MDAIWA; PHESTUS GELAD LWAMBUSHA**

**KWA; PHESTUS GELAD LWAMBUSHA WA DODOMA/SAE MBEYA**

**KK ITANGAZWE GAZETINI.**
**Kwa kuwa mdai/wadaiwa ameleta/wameleta madai yako/yao kwamba[Eleza hapa habari za mdaiwa kwa kifupi]**

NI JUU YA MADAI YALIYOPO MAHAKAMA YA MWANZO MWANJELWA MBEYA. Kwa hiyo unahitajiwa/unashitakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya JUMANNE tarehe 24/05/2022 saa 2;30 asubuhi/alasiri kwa kujibu madai haya na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinahusu shauri hilo kwa ajili ya kijitetea katika shauri hilo.Angalia kama hukuhudhuria siku hiyo iliyotajwahapo juu mahakama ikidhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/ameshindwa.Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 12/05/2022.

MAHAKAMA YA MWANZO
WILAYA YA MBEYA
HAKIMU WA MAHAKAMA YA MWANZO
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MWANJELWA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **HAMIS HASSAN KIBOI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI FUSO** yenye namba za usajili **T 107 BYS.** Yenye Chassis No: **FK416F520033** Na. Engine **No: 6D16601128** Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: **MUH/RB/1351/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JAZILA SAWAYA MSANGI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya T**OYOTA NOAH** yenye usajili namba **T380 CSE,** CHASSIS NAMBA **SR400224812,** ENGINE NAMBA **3S7942918.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/186376/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABDALLAH MWITA KITANO** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 114 CUD –** NISSAN VANETTE. Chassis namba **SK82VN336099.** Engine namba **F8EAA6099.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Control namba: **9910832857246.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAMOUD JUMA NDENGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T912AYA** aina ya Suzuki ESCUDO, yenye Chasis No.**TD11W113791,** Engine No. **H20A127027.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/145132/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HARSHID RAVIDRA DESAI,** anatangaza kupotelewa na Kadi ya Gari aina ya Nissan Langley yenye namba za usajili **T.809 ADS.** Yeyote atakayeiona atowe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi **MBE/MBE/RB/184321/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KAEN LUPAKISYO KAPANGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye NAMBA ZA USAJILI **T.311 CCN** aina ya **SUZUKI ESCUDO.** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/159676/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NATHALIE VAN DEN BERGE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **NISSAN X-TRAIL** yenye usajili namba **T400 CD 83,** CHASSIS NAMBA **PNT30002979,** ENGINE NAMBA **SR20602935W.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/180821/2022**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuweke utaalamu kwa timu za vijana

**KWA** hali ya kawaida kila klabu inapopambana kuhakikisha inaingiza timu yake kwenye Ligi Kuu inakuwa na malengo.

Zipo timu ambazo malengo yake ni kuwepo tu kwenye Ligi Kuu, hazina mpango wa ubingwa wala kucheza mashindano ya kimataifa. Hili ndilo kundi lenye timu nyingi, kwani humo humo ndimo hupatikana timu za kurudi Ligi ya Championships na hadi Daraja la Kwanza.

Malengo ya aina hii yana maeneo mawili. Moja ni nyenzo kwa maana ya rasilimali uchumi, kwani ili ucheze michuano ya kimataifa unahitaji mamilioni ya fedha.

Mfano ni gharama kubwa kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini vilevile ni faida kwa timu itakayofanikiwa kuwa bingwa kwani inapata fedha nyingi kuliko zile ilizotumia.

Hivyo kuna sababu za msingi kuingia katika mashindano ukiwa na malengo. Klabu inaweza kutumia nguvu nyingi kuhakikisha inacheza mashindano ya Afrika, lakini ikashindwa kusafiri kwenda kwenye mechi kutokana na kutokuwa na nguvu za kiuchumi.

Kwa Tanzania Bara tunao mfano wa timu za aina hiyo ambazo CAF hulazimika kuzipiga faini nzito.

Lakini bado timu inayo fursa ya kupigania ubingwa na kuupata, lakini baadaye ikasema haina uwezo kiuchumi kucheza mashindano ya CAF na nafasi yake kupewa timu inayoifuatia baada ya msimamo wa mwisho wa ligi. Eneo la pili ni la ufundi. Kwa mpira wa miguu, si klabu tu bali hata timu za taifa unapotafuta kocha ni lazima uje malengo ni nini vinginevyo ni wazi hakitatokea kile ambacho uongozi unakitarajia kuhusiana na matokeo ya uwanjani.

Katika timu 16 zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, kuna timu zenye makocha wa kigeni.Nini mchango wa makocha hao? Kwa haraka haraka waajiriwa hao (makocha) na waajiri wao wana sababu moja tu ya kuelezea mafanikio yao.

Pia wachezaji wa timu ya Taifa ya wakubwa (Taifa Stars) asilimia kubwa wanatoka katika klabu za ndani. Kwa lugha nyepesi ubora wa wachezaji katika klabu, hasa za Ligi Kuu ndiyo ubora wa timu za Taifa, hasa Taifa Stars.

Kwa vile mpira wa miguu ni biashara kubwa na nzuri, bado kuna kila sababu kwa klabu zetu kuwekeza zaidi kwa timu za vijana. Huku faida ni kubwa zaidi kuliko hasara.

Kuwekeza kwa vijana kunatoa fursa kwa wachezaji kupata msingi mzuri wa mpira wa miguu wakiwa bado wadogo.

Lakini vilevile kuwekeza huko kwenye vitalu ni biashara nzuri ingawa inahitaji kusubiri na uvumilivu wa kutosha ili kutoa mchezaji au wachezaji wanaoweza kupeleka faida katika klabu husika na pia timu ya Taifa.

Kuajiri makocha kwa ajili ya ubingwa tu hakuna faida kama kuwaajiri kwa ajili ya programu za vijana. Programu za vijana ni uwekezaji, na matunda yake yanachukua muda mrefu kuonekana, lakini pia yakishaonekana yatadumu kwa muda mrefu.

Mpira wa miguu kama ilivyo michezo mingine nguzo yake kuu ni kuwa na wachezaji ambao uwezo wao wa kucheza na kasi viwe ni vitu vinavyoongezeka badala ya kupungua. Kwa mantiki hiyo wanahitajika zaidi wachezaji vijana, kwani hao ndiyo miili yao inaruhusu wawe na kasi uwanjani.

Wachezaji wenye umri mkubwa au wakongwe wanahitajika kwenye timu kwa ajili ya ujuzi na uzoefu wao, lakini si kwa ajili ya kasi. Mpira wa miguu wa kisasa unahitaji kasi uwanjani, hivyo hilo haliwezi kuepukika kwa kocha yeyote.

Wastani wa umri wa wachezaji vijana katika timu unatakiwa kuwa angalau asilimia 70 dhidi ya 30 za wachezaji wakongwe na wazoefu. Nafasi za wakongwe nazo hujazwa na vijana baada ya muda mfupi.

Kwa mafanikio ya muda mfupi makocha wa mataji wanayo fursa katika mpira wa miguu Tanzania. Lakini kwa tulipo hivi sasa kwa hakika tunahitaji zaidi makocha wa maendeleo ya mpira wa miguu kuliko wale wa kuleta mataji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera CHAMUDATA, mna kazi kubwa

Na Adam Fungamwango

**HATIMAYE** Chama cha Muziki wa Dansi Tanzania kimepata viongozi wake watakaokiongoza kwa kipindi cha muhula mwingine, baada ya kupita miaka mingi bila ya kuwa na viongozi.

CHAMUDATA, chama kikongwe cha muziki nchini Tanzania, kilionekana ni kama kimekufa, kama ni kubebwa zaidi na Katibu Mkuu aliyemaliza muda wake, Hassan Msumari ambaye ilionekana kama yeye ndiye kila kitu, Mwenyekiti, Katibu na vyeo vyote. Kwa kiasi kikubwa anastahili sifa, kwani bila yeye sidhani kama hata baadhi ya watu wangejua kama kulikuwa na chama hicho.

Mwanamuziki, mwimbaji wa bendi ya African Stars 'Twanga Pepeta', Luiza Mbutu, ndiye Mwenyekiti mpya wa chama hicho kwenye uchaguzi uliofanyika wiki iliyopita jijini Dar es Salaam.

Mwanamuziki, mwimbaji na mtunzi wa bendi ya DDC Mlimani Park Orchestra, Abdallah Hemba, yeye alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti, huku nafasi ya Katibu Mkuu, ikienda kwa Katibu wa bendi ya Msondo Ngoma Music Band, Said Kibiriti.

Kuna wajumbe sita waliochaguliwa, na kwa kweli nitoe pongezi kwa waliotengeneza katiba ya chama hicho, kwani haikuwataka au kuwapendelea wanamuziki tu, bali hata wadau na wapenzi wa muziki wameruhusiwa kugombea.

Ndiyo maana hata baadhi ya Waandishi wa Habari za muziki na burudani kama Said Mdoe na wengineo wamechaguliwa kwenye nafasi ya ujumbe.

Hii inaonyesha kuwa chama hicho kinatambua kuwa ili muziki wa dansi uendelee si lazima kiongozwe na wanamuziki tu, bali hata wadau mbalimbali, wanaofanikisha kuutangaza na kuuenzi muziki huo.

Nilisikia kuwa moja kati ya mikakati ni kulinda maslahi ya wanamuziki wa dansi, ikiwemo kufuatilia mirabaha yao.

Hii ni kweli, chama sasa kinatakiwa kuendeshwa kisasa. Nyimbo hazipigwi redioni tu au kwenye mabaa, bali hata kwenye mitandao ya kijamii.

Muziki kwa sasa umehamia kwenye mitandao ya kijamii na huko ndiko hasa inatakiwa akili za viongozi zielekezwe na si kuzuia bendi ndogo kupiga laivu nyimbo za bendi zingine kubwa.

Nilisikia eti chama kinaambiwa kipige marufuku bendi ndogo kupiga nyimbo za bendi kubwa. Hii haipo duniani kote.

Wanamuziki wote unaowaona wakubwa, walianza kwanza kuiga kuimba na kupiga nyimbo za bendi na wanamuziki waliotangulia ndiyo wakawa hapo walipo.

Hata nchini Congo DR, JB Mpiana alianza muziki kwa kuiga nyimbo za Papa Wemba. Wenge Musica kwa miaka 10 wakati ikiwa bendi ndogo ilikuwa ikipiga nyimbo za kina Tabu Ley, Franco, Papa Wemba, Debaba na wengineo.Hakuna bendi yoyote duniani inayoweza kupiga muziki mwanzo hadi mwisho bila kupiga muziki wa bendi nyingine. Nadhani Luiza, na wenzake kwa sababu ni wanamuziki, wanalifahamu hilo. Acheni bendi ndogo na wanamuziki kupiga na kuimba nyimbo za watu wengine majukwaani, ili mradi tu wasirekodi.

Chama kina kazi kubwa ya kufanya kuliko hilo. Ni kuwarudishia kujiamini wanamuziki, pia kuiangukia serikali angalau kutengeneza studio, au ile ya TBC Dar na Dodoma, kuwapa unafuu wanamuziki wa dansi kurekodi kwa makubaliano maalum, kwani inavyoonekana tatizo kubwa la bendi za muziki wa dansi ni gharama ya kurekodi. Na ukiangalia hata studio wanazorekodi kwa sasa nadhani si nzuri, inawezekana ni za kurekodia muziki wa kisasa zaidi, kwani nyimbo za dansi hazitoki kwenye ubora kama ule wa nyimbo za zamani ambapo vifaa vilikuwa duni.

Nina uhakika kama bendi zitarejea kurekodi TBC, ambao wana studio zilizokamilika, kwa makubaliano maalum, muziki unaweza kurejea tena kwenye chati. Ni chama tu kukaa na serikali kushauriana, zirekodi bure kwa makubaliano ya kulipana watakapokuwa wanauza albamu zao.

Hiyo ndiyo kazi ya kufanya kwa Chamudata, ikiwemo sasa kuwa na mfuko wa kuwasaidia wanamuziki kama vile matibabu makubwa, siyo homa, maralia na tumbo, kifo, au matatizo ya kibinadamu mfano msaada kama wa kisheria kama akipatwa na tatizo lolote.

Mfuko huu unatakiwa kuchangiwa na wanamuziki wote wanachama wa Chamudata, lakini pia watengeneze mazingira pia ya wanamuziki au wadau ambao si wanachama wanaotoa michango yao pia kusaidiwa.

Wanamuziki wengi walionekana kujitokeza kwenye uchaguzi, hii inaonyesha kuwa wanataka sasa mabadiliko na wanataka kuona chama chao kinafanya mambo ambayo hata wao watajivunia kuwa nacho, pia watajivunia kuwa wanamuziki au wadau wa muziki.



Mkuu wa mkoa wa Iringa, Queen Sendiga (wa pili kulia), akikabidhi hati ya umiliki wa ardhi kwa mkazi wa Mlandege, Zawadi Mgongolwa, mkoani humo juzi. Zaidi ya hati 170 zilitolewa kwa wakazi wa manispaa ya Iringa. Wanaoshuhudia ni Mkuu wa wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo (wa tatu kulia) na (kulia) ni Kamishina Msaidizi wa Ardhi wa mkoa huo, Wenslaus Mtui. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## Mbivu, mbichi kesi vigogo CWT Mei 23

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, inatarajia kutoa uamuzi wa kesi ya matumizi mabaya ya madaraka inayomkabili aliyekuwa Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Deus Seif, na Mtunza Hazina Abubakar Allawi, kama wana kesi ya kujibu au la Mei 23, mwaka huu.

Mahakama hiyo ilifikia hatua hiyo jana baada ya upande wa mashtaka kufunga ushahidi wao wa mashahidi tisa na vielelezo 11 mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate.

Kesi hiyo kwa upande wa mashtaka, iliongozwa na Wakili Imani Nitume ambaye aliwaongoza mashahidi hao mahakamani kutoa ushahidi dhidi ya washtakiwa.

Seif na Allawi wanakabiliwa na mashtaka mawili ya matumizi mabaya ya madaraka na kujipatia zaidi ya Sh. milioni 13 kinyume cha sheria.

Katika kesi hiyo, inadaiwa kuwa washtakiwa walitenda makosa hayo kati ya Oktoba 3 hadi Novemba 6, 2018 jijini Dar es Salaam. Ilidaiwa kwamba washtakiwa wakiwa watumishi wa CWT, walitumia madaraka yao vibaya na kujipatia Sh. 13,930,963 kwa manufaa yao. Katika shitaka la pili, ilidaiwa kuwa katika tarehe na eneo hilo, washtakiwa walichepusha kiasi hicho cha fedha mali ya CWT kwa kutumia nafasi walizo nazo.

## Waziri atafutia ufumbuzi mkwamo malori ya mizigo

**Na Benny Mwaipaja**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema serikali itawasiliana na Mamlaka za Kenya ili kutatua changamoto ya malori ya mizigo yanayovuka kupeleka bidhaa nchini humo kutumia muda mrefu kupata vibali vya kuvuka mpaka wa Horohoro.

Dk. Nchemba alisema hayo baada ya kuzungumza na madereva wa malori yanayobeba mizigo kwenda Kenya katika mpaka wa Horohoro, akiwa njiani kwenda Mombasa nchini Kenya kwenye mkutano wa Mawaziri wa Fedha wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Madereva hao walisema wanapata usumbufu mkubwa kwa sababu wanatumia takriban siku 14 hadi 21 kuvuka mpaka wa Horohoro kwenda Kenya, wakati madereva wa Kenya wanaoingia Tanzania wanatumia siku tatu kuvuka mpaka huo.

Walisema kuchelewa kuvuka mpaka kunawaletea matatizo makubwa ikiwamo kutumia gharama kubwa zisizolingana na posho za safari wanazopewa na waajiri wao, lakini pia kuna baadhi ya bidhaa zinaharibika kabla ya kuvuka mpaka. Dk. Nchemba alisema amebaini kuwa ucheleshwaji wa huduma ya forodha kwa Kenya unatokana na nchi hiyo kutoanza kutumia Mfumo wa Pamoja wa Huduma ya Forodha kama walivyokubaliana.

Alisema kuwa magari ya Kenya hayapati changamoto hiyo ya foleni kwa kuwa tayari Tanzania wanatumia mfumo huo na mizigo yote ya Kenya hupata vibali kabla ya kufika katika mpaka na malori kupita bila tatizo.

Dk. Nchemba alisema atawasiliana na waziri mwenzake wa fedha wa Kenya ili kuanza kutekeleza makubaliano ya kuweka mfumo huo wa pamoja na forodha kwa kuwapeleka watumishi wa nchi hiyo upande wa Tanzania ili kuharakisha usafiri na usafirishaji wa mizigo kutoka Tanzania.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuwaondolea adha wafanyabiashara na madereva wanaotumia mpaka huo kufanya biashara zao.

## TAMWA yamshukuru Rais Samia waliopata mimba kurejea shuleni

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), kimemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuridhia watoto wa kike waliopata ujauzito kurejea shuleni kuendelea na masomo.

Mkurugenzi Mtendaji TAMWA, Dk. Rose Reuben, alitoa pongezi hizo jana mkoani Dar es Salaam katika maadhimisho ya miaka 10 ya Muungano wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), ambayo Rais Samia alikuwa mgeni rasmi. "Tunaishukuru serikali ya awamu ya sita, mwaka jana iliridhia na kuruhusu watoto wa kike ambao wamepata ujauzito baada ya kujifungua kurejea tena shuleni kuendelea na masomo, hili ni jambo zuri," alisema Dk. Reuben.

Alisema mimba za utotoni zimekuwa zikitokea kwa sababu nyingi ikiwamo ndoa za utotoni, malezi mabaya kwa watoto wa kike, ubakaji ama makosa ya kibinadamu. Dk. Reuben alisema katika kipindi cha miaka 10 ya THRDC, TAMWA imeendelea kupinga kwa kiwango kikubwa ukatili wa kijinsia kwa wanawake, wasichana, watoto na wanaume.

"Wanawake watu wazima na wenyewe wana haki zao na hata wanawake wazee wana stahiki zao na wanapokuwa na haki zao maana yake wanahitaji kulindwa na kutetewa," alisema.

Katika kipindi hicho, alisema TAMWA imeendesha kampeni ya kupinga mauaji ya wanawake wazee ambayo yalifanyika mkoani Shinyanga na maeneo mengine kwa kuwatuhumu kufanya uchawi.

Dk. Reuben alisema suala la mila potofu ni kampeni waliyoianzisha kwa ajili ya kuzuia ukatili kwa wanawake ambao wanafanyiwa.

Alisema pia walifanya kampeni ya kutungwa sera na adhabu kali kwa wale wanaotekeleza mila potofu ikiwamo kuozesha watoto katika umri mdogo, ubakaji na mimba za utotoni.

Naye Mraribu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, aliiomba serikali kuwapo na sheria au sera za kuwatambua watetezi wa haki za binadamu.

# Watalii waongezeka fukwe za bahari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Maliasili na Utalii imesema idadi ya watalii imeongezeka kwenye fukwe za mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, , Mary Masanja, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum, Tunza Malapo, aliyehoji serikali ina mkakati gani wa kukuza utalii katika fukwe za bahari nchini.

Akijibu swali hilo, Masanja alisema serikali imeendelea kubuni mikakati mbalimbali ya kuendeleza mazao mbalimbali ya utalii, ikiwamo utalii wa fukwe.

Katika kutekeleza mikakati hiyo, alisema idadi ya wanaotembelea fukwe zetu zilizopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara imeendelea kuongezeka.

Alisema serikali imebaini maeneo mapya ya fukwe za Bahari ya Hindi yanayofaa kwa ajili ya uwekezaji wa shughuli za utalii katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara.

Pia alisema kuweka utaratibu wa kusajili maeneo ya fukwe yanayofaa kwa shughuli za utalii kama Maeneo Maalum ya Uwekezaji wa Shughuli za Utalii (Tourism Special Economic Zones).

"Kuendelea kuwahamasisha wamiliki wa maeneo ya fukwe nchini ili kusajili maeneo ya fukwe wanayoyamiliki chini ya utaratibu wa maeneo maalum ya uwekezaji wa shughuli za utalii kwa lengo la kuiwezesha serikali kushirikiana na wamiliki hao kuhimiza uwekezaji wa utalii wa fukwe.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akijadiliana jambo na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi mstaafu ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Jenerali Davis Mwamunyange, walipokutana Bungeni jijini Dodoma juzi, wakati wa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2022/2023. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Magogoni, Gezaulole wapata ahueni maji

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa mitaa ya Magogoni, Soko Maziwa na Gezaulole, Kata ya Kigamboni mkoani Dar es Salaam, wamenufaika na huduma ya maji baada ya kazi ya kusogeza huduma iliyofanywa kukamilika.

Kazi hiyo ilifanywa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) katika mkoa wa kihuduma wa Kigamboni.

Mhandisi wa Miradi wa DAWASA Kigamboni, Mohamed Nondole, alisema kazi ya kusogeza huduma imefanyika kwa lengo la kuwezesha huduma kufika kikamilifu kwa wakazi wa mitaa hiyo ambao awali hawakuwa wamefikiwa na huduma.

Alisema kazi hiyo imehusisha ulazaji wa mabomba ya inchi mbili kwa umbali wa mita 998 kwa mtaa wa Magogoni na kuhudumia zaidi ya wakazi 50.

Kwa Mtaa wa Soko Maziwa, Mhandisi Nondole alisema mradi umelaza mabomba ya inchi mbili kwa umbali wa mita 550 kwa lengo la kuhudumia zaidi ya wakazi 20 na kwa mtaa wa Gezaulole, mradi umelaza mabomba ya inchi 1.5 kwa umbali wa mita 150 ili kuhudumia wakazi wapatao 20.

"Kazi ya kusogeza huduma imekamilika na sasa wakazi wa mitaa hiyo wanapata huduma ya maji safi vizuri," alisema.

Mhandisi Nondole alifafanua kuwa kazi ya kusogeza huduma kwenye mitaa tajwa imefanyika kwa kutumia chanzo cha maji ya Mto Ruvu kwa Mtaa wa Magogoni na Soko Maziwa, ambapo kwa Mtaa wa Gezaulole, mradi umepeleka maji kupitia chanzo cha maji ya kisima cha Geza.

Mmoja wa wanufaika wa huduma hiyo, Agnes Shija, ambaye ni mkazi wa Mtaa wa Magogoni, aliishukuru DAWASA kwa kusogeza huduma karibu na makazi yake kwa kuwa alikuwa anapata usumbufu mwingi wa kuchota maji kwa majirani walioko mbali.

"Ilinilazimu kwenda kuomba maji kwa watu kila wakati, kama hawapo inabidi nichote maji ya kisima kuja kwa huduma hii nyumbani kwangu ni nafuu kubwa maana itanipunguzia adha ya kutafuta maji mbali," alisema Shija.

Naye Hadija Ramadhani ambaye ni mkazi wa Soko Maziwa, alisema ni jambo la muhimu kwa huduma kufika karibu na makazi yao kwani inapunguza muda mwingi waliokuwa wakiutumia kutafuta maji.

"Naiomba DAWASA iboreshe huduma maji yasiwe ya kukatika mara kwa mara na bila taarifa na idhibiti tatizo la vishoka wanaowarubuni wateja," alisema.

# Kanuni mpya zawawezesha wenye simu kutumia bando hadi mwisho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imefanya mabadiliko ya kanuni ili kuwezesha wananchi kutumia bando mpaka mwisho.

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Andrea Kundo, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Salome Makamba.

Katika swali lake, Makamba alisema kutokana na tatizo la mtandao kutoka na kurudi wananchi wamekuwa wakipata tatizo la kuisha muda wa bando hata kama hajatumia.

"Nataka kujua kama serikali haioni haja ya kubadili utaratibu wa matumizi ya bando badala ya kuisha kutokana na muda na badala yake liishe kutokana na matumizi,"alisema.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kundo alisema serikali imebadili kanuni ambazo zinatoa fursa ya kutumia bando mpaka mwisho.

Alisema mabadiliko hayo yametoa maelekezo ya kuwa miradi inayotekelezwa iwe na uwezo wa kutoa huduma ya intaneti.

Pia alisema serikali imeweka utaratibu wa mwananchi ambaye bando lake linakaribia kuisha basi atalihamisha au kulipeleka mbele.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Urambo (CCM), Margaret Sitta, alitaka kujua ni lini serikali itajenga minara katika maeneo ambayo hayana minara na kutatua matatizo ya mawasiliano katika maeneo yenye minara.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kundo alisema serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) inatekeleza miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano katika kata tatu za Ugalla, Itundu (Mpigwa) na Vumilia wilayani Urambo na ujenzi wa minara unaendelea na utakamilika ifikapo Julai, mwaka huu.

Serikali, alisema imepanga kufikisha huduma za mawasiliano ya simu Kata za Kiloleni, Kasisi, Itundu (Itundu) na Uyogo katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 baada ya kubaini uwepo wa changamoto za mawasiliano katika baadhi ya maeneo ya vijiji katika kata hizo.

"Kata hizo zimejumuishwa katika zabuni inayotarajiwa kutangazwa kabla ya mwaka wa fedha wa 2021/2022 kukamilika kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali," alisema.

Alisema utekelezaji wa miradi hiyo ya usimikaji wa minara ya mawasiliano utahusisha uboreshaji wa mawasiliano ili kukidhi mahitaji ya upatikanaji wa huduma za intaneti katika Kata za Songambele na Imalamakoye.



## HABARI DODOMA

# 860 wajitosa MAKISATU

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNIFU 862 wamejisajili kushiriki Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU 2022).

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, anatarajia kuzindua maadhimisho ya Wiki ya Ubunifu ya mwaka 2022 yatakayokwenda sambamba na mashindano hayo.

Akizungumza jana jijini hapa, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema Rais Mwinyi atafanyia uzinduzi huo Mei 16 mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma.

Alisema wabunifu waliosajiliwa ni kutoka makundi ya shule za msingi 38 na shule za sekondari (273), vyuo vya ufundi stadi (36), vyuo vya kati (124), vyuo vikuu (127), taasisi za utafiti na maendeleo (30) na mfumo usio rasmi (234).

"Mbali na fainali za MAKISATU kutakuwa na maonyesho mbalimbali ya ubunifu na teknolojia za wabunifu wa Kitanzania, maonyesho ya huduma na bidhaa zinazotolewa na taasisi mbalimbali nchini, maonesho yanatoa fursa kwa wabunifu au wagunduzi kujitangaza na kujulikana kwa wawekezaji, watumiaji wa bidhaa zao na wadau wengine wa ndani na nje ya nchi," alisema.

Prof. Mkenda alisema kutakuwa na mijadala, warsha na mafunzo kuhusu sayansi, teknolojia na ubunifu itakayowahusisha wabunifu, watafiti, watunga sera, taasisi za umma na binafsi, washirika wa maendeleo, wadau wa ubunifu na wataalamu mbalimbali.

Alisema wiki hiyo pia imeadhimishwa katika ngazi ya mkoa kwa kufanyika mikoa 16 kuanzia Aprili 27 mwaka huu na kufikia tamati yake leo (Mei 14).

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Iringa, Mwanza, Unguja Magharibi, Tanga, Kilimanjaro, Morogoro, Njombe, Kagera, Mtwara, Kigoma, Mara na Ruvuma.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2019 hadi mwaka 2021, wizara imeibua na kuwatambua wabunifu wachanga 1,785.

"Kazi za ubunifu 466 zilikidhi vigezo baada ya kutambuliwa na kuhakikiwa na kati ya hizo, kazi za ubunifu mahiri 200 tayari zinaendelezwa na serikali ili kufikia hatua ya kuwa za kibiashara," alisema.

Aliongeza kuwa hadi kufikia mwaka 2021 kati ya kazi za ubunifu zinazoendelezwa na serikali ni 26 zimefikia hatua ya kuwa za kibiashara na 95 zipo katika hatua ya uundaji wa sampuli kifani yenye uwezo wa kufanya kazi na nyingine katika hatua ya majaribio ya sampuli kifani katika mazingira yenye uhalisia.

# TBS yapata cheti cha kimataifa utoaji huduma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limepokea cheti cha kimataifa cha ithibati cha utoaji huduma uthibitishaji wa mifumo ya kimenejimenti huku taasisi za umma na sekta binafsi zikitakiwa kuthibitisha mifumo yao.

Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Exaudi Kigahe, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye hafla ya kupokea cheti hicho kutoka Huduma za Ithibati za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADCAS).

Alisema ithibati ina manufaa makubwa kwa taasisi za umma na binafsi na TBS inatoa huduma kwa gharama nafuu kulinganishwa na gharama zinazotozwa na kampuni za nje ambazo zimekuwa zikitoa huduma hizo.

"Hivi karibuni, kampuni ya nje yamepata changamoto kutokana na janga la UVIKO-19 na hivyo kushindwa kutoa huduma kwa wateja wao, hali iliyosababisha wateja wao kupoteza uhalali wa kuwa na vyeti vya uthibitisho wa mifumo ya kimenejimenti," alisema.

Naibu waziri huyo alisema kutokana na tatizo hilo, baadhi ya taasisi tayari zimefanya uhamisho wa kupata huduma ya uthibitisho wa mifumo ya kimenejimenti kutoka kampuni za nje kwenda TBS ili kunufaika na huduma ya uhakika kwa gharama nafuu.

"Niwapongeze TBS kwa kufikia hatua hii kubwa ya kupata ithibati ya umahiri katika kutoa huduma ya ithibati ya umahiri katika kutoa huduma hii, sina shaka mtaendelea kudumisha na kuongeza wigo kwenye kutoa huduma zenye ithibati ya umahiri ili kukuza uchumi na kuleta maendeleo kwa taifa," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa SADCAS, Victor Mundembe, aliitaka TBS kuhakikisha inazingatia ubora kwenye utoaji huduma hizo ili viwango vya ithibati hiyo visishuke.

"Kama tutabaini viwango vinashuka, tutawanyang'anya hii ithibati," mkurugenzi huyo alitoa angalizo.

Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora TBS, Lazaro Msasalaga, alitaja hatua mbalimbali za kupata cheti hicho kuwa ni pamoja na kuweka na kufuata mifumo kulingana na matakwa yaliyoainishwa kwenye kiwango cha kimataifa ISO/IEC 17021.

"Kujipima utendaji kwa mujibu wa kiwango husika pamoja na matakwa ya tume ya ithibati na kuwa na wataalamu wenye umahiri na weledi katika dhana nzima ya utoaji huduma," alifafanua.



Waziri wa Ujenzi naUchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akizungumza na Mkurugenzi wa kampuni ya GF Trucks & Equipment's Ltd, Salman Karmal, wakati wa mkutano wa Bodi ya Makandarasi nchini, ulioandaliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), jijini Dodoma juzi. Katikati ni Mwenyekiti wa Bodi ya Makandarasi nchini, ConsolataNgimbwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango kazi kizazi chenye usawa waiva

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya kitaifa ya ushauri na uratibu wa utekelezaji wa ahadi za nchi katika Jukwaa la Kizazi chenye usawa inatarajia kukamilisha rasimu ya mpango kazi wake Juni mwaka huu ili upelekwe kwenye vikao vya juu vya uamuzi.

Akifungua juzi kikao cha kamati hiyo kilichokuwa kinapokea rasimu ya mpango kazi wa utekelezaji wa ahadi hizo jijini hapa, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema mpango kazi huo utakapokamilika utaonyesha tathmini ya hatua ambazo tayari nchi imepiga katika utekelezaji ajenda ya usawa wa kijinsia na maeneo ya kutilia mkazo.

Dk. Gwajima alisema kamati ikifanya kazi kwa bidii katika kuhakikisha ahadi za nchi zinatekelezwa katika jukwaa, utakuwa ni mwanzo wa kizazi chenye usawa na kuwa nchi ya mfano wa kuigwa.

"Rais amedhamiria kuhakikisha nchi inakwenda sambamba na ulimwengu na haimwachi mtu nyuma kwa visingizio vyovyote hasa wanawake walioachwa nyuma kwa miaka mingi ambako kumesababisha maendeleo duni kwa watoto wa kiume na wa kike, hivyo tunapaswa kuhakikisha mlolongo huo tunaumaliza ili jamii yote tuwe na kizazi cheye usawa na kuongeza kasi ya maendeleo maradufu," alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, alisema kamati hiyo tangu iteuliwe imekuwa na ushirikiano mkubwa na wizara katika kuhakikisha matarajio ya nchi yanafikiwa.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Angellah Kairuki, alisema rasimu hiyo itakuwa na ubora na utaakisi mazingira ya Tanzania bila kumwacha mtu yeyote nyuma.

Alishukuru wizara kwa ushirikiano katika kufanikisha kuwa na rasimu ya mpango kazi utakaotumiwa na kamati hiyo kufanya kazi yake ya kuratibu ahadi za nchi kufikia kizazi chenye usawa.

"Malengo yetu ni kuwa na mpango mkakati unaokidhi mazingira ya nchi yetu na usiomwacha mtu nyuma, tangu Desemba mwaka jana kamati imeshafanya vikao vinne kwa ajili ya kupitia rasimu ya mpango kazi huu na sasa tupo tayari kupokea," alisema.

Kairuki aliongeza kuwa hatua zinazofuata ni kuwa na vikao kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar ambako kamati itakutana na wadau wa mbalimbali kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali, sekta binafsi, viongozi wa dini, makundi maalum, wasanii, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar (ZATUC), vijana na vituo vya ubunifu.

Mnamo Desemba 16 mwaka 2021, Rais Samia Suluhu Hassan aliiteua kamati hiyo kwa lengo la kushauri na kuratibu utekelezaji wa ahadi za nchi katika Jukwaa la Kizazi chenye Usawa, ambapo Rais alichagua kutekeleza eneo la pili la kuhakikisha usawa wa jinsia.



# Hemed ahimiza ubora wa miradi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewaagiza wataalamu wa Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi kuipitia na kukagua miradi wanayoisimamia ili iwe ya viwango bora.

Hemed alisema hayo jana katika ziara yake ya kukagua ujenzi wa boti za uvuvi zinazojengwa kwa fedha za kupunguza athari za UVIKO -19.

Alisema kusimamia ubora wa boti hizo ni jambo la msingi na ni jukumu la wataalamu kushirikiana na makandarasi kuhakikisha ubora huo kwa usalama wa wananchi kwa mujibu wa mikataba ya ujenzi.

Hemed alisema dira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kukuza uchumi wake kupitia sekta ya uchumi wa bluu na kwamba kukamilika kwa boti hizo kutatoa taswira ya kufikia uchumi huo sambamba na wananchi wengi kunufaika kwa kupitia sekta hiyo.

"Boti hizi zikikamilika wananchi wataona kwa vitendo azma ya serikali katika kukuza uchumi wake kupitia uchumi wa bluu pamoja na kujikwamua kiuchumi," alisema Hemed.

Makamu wa Pili huyo alisema serikali haitopokea boti yoyote iliyo chini ya kiwango na kwamba mkandarasi yeyote atakaekabidhi boti zisizo na kiwango atalipa kwa gharama zake bila kuitia hasara serikali.

Pia alisema utengenezaji wa boti hizo 500 ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 ambapo serikali imeamua kuendelea kuisimamia kwa vitendo kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa Zanzibar.

Katika ziara hiyo, Hemed alieleza kufurahishwa na hatua ya kampuni ya Qiro Group kwa kukamilisha ujenzi wa boti 250 ilizokabidhiwa na Wizara ya Uchumi wa Bluu kabla ya kufikia muda uliokubaliwa kwa mujibu wa mkataba.

Aliuagiza uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi kuhakikisha inakamilisha taratibu zilizobaki na kumlipa mkandarasi huyo ili kukabidhiana boti hizo na zianze kutumika.

Naye Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, alisema ujenzi wa boti 250 zilizojengwa na Kampuni ya Qiro umeshakamilika na mtaalamu wa wizara ameshakagua na kutoa uhakika wa ubora wa Boti hizo ambapo wizara kwa sasa inasimamia malipo pamoja na kukabidhiwa.

Pia alisema wizara yake itaendelea kusimamia ubora wa boti zote zinazojengwa ili kufikia malengo ya serikali kuwasaidia wananchi wake kwa huduma bora na zenye kiwango.



Waziri wa Biashara na Viwanda Zanzibar, Omar Said Shabani, akiwasilisha bajeti ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2022/2023, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Hali ya biashara yazidi kuimarika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Omar Said Shaaban, amesema hali ya biashara imeendelea kuimarika kwa kipindi cha mwaka 2021.

Amesema katika kipindi hicho , Zanzibar imefanya biashara yenye thamani ya Sh. trilioni 1.12 ikilinganishwa na Sh. bilioni 913.09 kwa mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 23.1.

Akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/23 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana, alisema biashara hiyo ilikuwa usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya Zanzibar na uagiziaji wa bidhaa kuingia Zanzibar.

Waziri Omar alisema mwaka wa fedha 2021/22 Zanzibar imeagiza bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 7.823 kutoka nchi za kusini mwa Afrika, ambayo ni sawa na asilimia 0.8 ya uagiziaji wote.

"Uagiziaji wa bidhaa kwa nchi za SADC kwa mwaka 2021 umeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 6.15 ziliagizwa," alisema.

Alisema Afrika Kusini imeongoza kwa kuingiza bidhaa Zanzibar zenye thamani ya Sh. bilioni 6.88 kwa mwaka 2021 kwa bidhaa za nguzo za mbao.

Pia alisema kwa mwaka wa fedha 2021/22 Zanzibar imesafirisha nje bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 155.62, kiwango hicho cha usafirishaji ni sawa na ongezeko la asilimia 137 ikilinganishwa na usafirishaji wa bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 65.66 uliofanyika kipindi cha mwaka 2020.

Alisema bidhaa zilizosafirishwa nchi za nje ni pamoja na karafuu, mwani na mazao ya baharini na katika usafirishaji huo, zao la karafuu lilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 115.36 sawa na asilimia 74.1 ya usafirishaji wote.

" Ongezeko hilo limechangiwa na kupanda kwa bei ya karafuu na msimu mkubwa wa uzalishaji. Miongoni mwa nchi zilizonunua karafuu ni pamoja na Singapore, India, Denmark na nchi za Falme za Kiarabu (UAE)," alisema.

# Zanzibar kukopa Dola milioni 33 kuimarisha kilimo mpunga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imejipanga kuinua kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula na inakusudia kukopa

Dola milioni 33 za Marekeni katika taasisi za fedha za kimataifa.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi kuhusu hoja zilizoibuliwa na wajumbe kuhusu maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji cha mpunga.

Dk. Mohamed alisema serikali inakusudia kukopa Benki ya Dunia Dola milioni 15 ambazo zitatumika katika kuimarisha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji.

Pia alisema alisema serikali inakusudia kukopa kupitia Benki ya Exim Dola milioni 18 ambazo zitatumika katika uimarishaji wa kilimo cha mpunga ambacho kitahusisha utoaji wa wa elimu kwa mabibi shamba na mabwana shamba vijijini Unguja na Pemba.


Alibainisha kuwa fedha hizo zitatumika katika kuimarisha hekta 1,000 za mpunga katika mabonde 10 Unguja na Pemba hatua ambayo imelenga kuongeza uzalishaji wa kilimo cha umwagiliaji maji.

"Mheshimiwa Spika hiyo ndiyo mikakati ya Serikali ya Mapinduzi katika kuimarisha kilimo cha umwagiliaji hatua ambayo inakwenda sambamba na mikakati ya kujitosheleza kwa chakula," alisema.

Alisema hayo ni maelekezo ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ambaye mikakati yake inayotokana na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM, imejikita katika kujitosheleza kwa chakula.

Kilimo cha umwagiliaji, alisema kimeshuka uzalishaji wake kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya tabianchi ambayo yamefanya kupungua kwa mahitaji ya mvua.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walitishia kuzuia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji baada ya kudai kwamba uzalishaji wa kilimo cha umwagiliajichampungahaukupewa kipaumbele katika mwaka ujao wa fedha.



WEMA
UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI MEI 14, 2022



# JUDITH NGUSA Ushindi Miss United Nations wachambuliwa

BAADA ya kutangazwa Mtanzania Judith Ngusa, kuibuka mshindi katika shindano la urembo la Miss United Nations 2022, baadhi ya wachambuzi wanasema bado kunahitajika usahihi wa suala hilo.

Judith ambaye ni mshindi wa pili Miss Utalii Tanzania 2021, aliibuka mshindi wa kwanza katika fainali za dunia za Miss United Nations zilizofanyika New Delhi India.

Hata hivyo, baadhi ya wachambuzi wanasema taarifa hizo ambazo zinailetea sifa taifa, lazima kuna mambo hayajakuwa sawa kutokana na ukubwa wa shindano hilo.

Karim Hassan, amesema watu waliohusika kumpeleka mrembo huyo kuwania shindano hilo, wangehakikisha wanakuwa na picha ambazo Judith anaonekana akivishwa taji jukwaani.

“Watanzania tumefurahishwa na jambo hili, lakini wametunyima raha zaidi kwa kutoonyesha mrembo wetu akivishwa taji jukwaani kuliko kutuambia na kutuacha hewani,” amesema Karim.

Amesema kiujumla anamwagia sifa Judith kwa kufanya vizuri na kuomba atafutiwe nafasi nyingine kwa kushiriki mashindano makubwa zaidi.

Awali ilielezwa kuwa kwa ushindi huo Judith ameendeleza rekodi ya Tanzania ya kushinda mataji katika fainali za Dunia, Judith Peter, anakuwa ni Mrembo wa Saba wa Miss Utalii Tanzania kushinda mataji mbalimbali katika fainali za Dunia.

BASI SAWA

## Carly Boy atambulisha lebo yake



Msanii anayekuja kwa kasi kwenye Bongo Fleva, Ismail Npangafinyu, maarufu kama Carly Boy, ameweka wazi lebo yake mpya inayoitwa Doni Mone Records.

Akizungumza na BT jana, Carly Boy amesema licha ya kuwa bado ni msanii mdogo lakini ana maono makubwa ya kusaidia wasanii wachanga kupitia lebo hiyo iliyopo maeneo ya Sinza, jijini Dar es Salaam.

"Nimeona niweke wazi kuhusu lebo yangu ya Doni Mone Records ambayo natamani iwasaidie vijana wengi, bado naomba sapoti kwa mashabiki nimeachia wimbo wangu mpya unaoitwa Kaona," amesema Carly Boy

## Mbosso uliona wapi mapenzi kama muwa?



MAONI ya mwanamuziki wa Bongo Fleva, Mbosso Khan kuhusu furaha ya kuwa na wapenzi wanne, imeibua mitazamo tofauti kutoka kwa wafuasi wake.

Wiki hii, Mbosso ameeleza kwamba mtu ukiwa na mpenzi mmoja anakupa furaha, vipi ukiwa na wapenzi wanne kwa wakati hizo furaha zake.

Baadhi ya watu walimjibu kuwa mapenzi hayana idadi na badala yake kuridhika, na wengine walikwenda mbali na kuhoji pengine mkali huyo wa muziki ana uhusiano wa kimapenzi na wanawake zaidi ya mmoja kwa sasa.



## Wema umekuwa jalala, vumilia yataisha

MWIGIZAJI mkongwe wa Bongo Muvi, Wema Sepetu ameonekana kukasirishwa kwa kitendo cha Bob Junior, ambaye alijigamba kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na mrembo huyo na ana mpango wa kumtolea mahari.

Wema kupitia ukurasa wake wa Instagram, alikanusha kuwa ana uhusiano na msanii huyo wa muziki akisema hakumamini kile alichokisikia.

"Umenikatisha tamaa Bob Junior kwa sababu maisha yangu nimekuwa nikikuchukulia kama rafiki na nimekuwa nikimkubali kama mwana, sasa sielewi ndugu yangu ukala nini au umeona ni sawa kwenda kuongea kuwa mimi ni mwanamke wako?"amehoji wema.

# Dereva Taxi: Mapenzi hayaonjwi kama njugu

**Na Adam Fungamwango**

WA zamani walisema mapenzi upofu. Wengine wakasema mapenzi ni fumbo la hiyari.

Pia wako waliosema mapenzi hayajaribiwi. Ni kweli kabisa, kujaribu mapenzi ni jambo la hatari sana.

Ni kwa sababu wakati mwingine huingia taratibu moyoni mwa mtu. Mara ya kwanza ukimuona mtu unamtamani, humpendi, lakini kadri muda unavyozidi kusonga mbele, ndiyo mapenzi yanapokuja.

Kama hakuna mapenzi, kutamani kunakinai.

Tunayaona haya kwenye filamu ya 'Dereva Taxi'. Imechezwa na baadhi ya wasanii maarufu mama Jacob Steven JB, Jackline Wolper, Mzee Chilo na wengineo.

JB ni dereva taxi, na katika pitapita yake usiku anakutana na vijana wa kihuni wakitaka kumbaka msichana, akaamua kumuokoa.

Anampeleka nyumbani kwake. Lakini hilo linamgharimu, kwani msichana anasahau simu, ambayo inaingia kwenye maji na kuharibika.

JB anapojaribu kumtafuta, akamrudishia ikiwa mbovu anageukwa na kuambiwa alipe. Pesa hana, anapewa kazi ya kumtembeza msichana huyo kufidia gharama hizo, kwani simu hiyo ilikuwa ni ya shilingi laki sita.

Msichana huyo ni Wolper, ambaye ni denti wa chuo, lakini 'aliyepinda'. Ni denti anayeyajua ya usiku na ya mchana, yeye na klabu, klabu na yeye.

Ni siku chungu kwa JB, kwani alilazimika kumpeleka popote anapotaka. Baada ya kuona maendeleo ya binti yake si mazuri darasani, baba yake Wolper anaamua kutaka kumpeleka nje ya nchi.

Hii inamfanya binti huyo kumuingiza JB kwenye mtego wa kujifanya ni anataka kumuoa, ili dili la kwenda nje life, asomee hapa hapa.

Baada ya majadiliano ya muda mrefu, JB anakubali kwa shingo upande. Awali inakuwa vigumu kwa mzee Chilo kukubali hilo kutokana na hali duni ya mkwewe mtarajiwa, lakini baadaye anakubali, lakini kwa masharti na kumtafutia kiasi fulani cha pesa ambacho kwa JB ni mtihani mkubwa.

'Uchumba feki' unamchosha Wolper na kuamua kumwambia ukweli baba yake kuwa alimdanganya kwa sababu asiende nje ya nchi.

Wakati anaongea hivyo, JB anaingia akiwa na kiasi cha pesa alichoambiwa na mzee Chilo, anamkabidhi.

Anaposikia kuwa 'dili limebumburuka', JB anaondoka kwenye kasri la mzee Chilo. Siku moja baadaye akiwa kijiweni na wenzake, Wolper anakuja na Taxi mpya kabisa. Anamkabidhi JB na kumwambia amepewa na baba mkwe wake.

Kile kiasi kidogo alichopeleka, mzee ameongezea na kununua gari ambalo amempa JB, ili sasa amkabidhi binti yake amuoe. JB na Wolper wakaacha usanii, sasa wakawa wachumba rasmi.

Kumbe kuwa wote kwa muda mrefu, kila mmoja akaanza kumhusudu mwenzake.





## Harmonize atamani kupima DNA

MWANAMUZIKI Harmonize, amebeba jukumu kama mzazi , baada ya kumshauri msanii mwenzake Ibraah kwenda kufanya vipimo vya DNA ili kujua uhalali wa mtoto anayedaiwa kuwa ni wake.

Hivi karibuni kumesambaa mitandaoni picha za mtoto na mwanamke anayedaiwa amezaa na Ibraah, huku mwenyewe akikana kuwa na mtoto.

"Kaka tuletee huyu mfalme tutakopa, tutaiba ili mradi mkono uende kinywani, nenda tu ukajiridhishe na DNA upate amani ya moyo ila huyu Chinga.." ameandika harmonize.

## KALI 5 ZILIZOTAMBA APRILI

**Na Adam Fungamwango**

HUU ni mwezi Mei ambapo mashabiki wa muziki wa bongo fleva bado wanaendelea kufurahia, kucheza na kuimba ngoma kali zilizoachiwa mwezi Aprili.

Kuna ngoma kibao zimeachiwa mwezi uliopita, lakini kuna hizi kali ambazo zimeteka hisia na nyoyo za mashabiki wa muziki huo.

Zinapigwa kwenye mitandao ya kijamii, vituo vya televisheni na redio pia. Hebu tuzitazame ngoma hizo.

**Samia Suluhu-Diamond Platnumz**

Ilikuwa ni Aprili 12, msanii Diamond Platnumz alipoachia ngoma iitwayo 'Samia Suluhu', maalum kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kutokana na uongozi wake bora, tangu aanze kushika usukani Machi mwaka jana.

Kwenye ngoma yake hiyo, msanii huyo maarufu nchini amemtaja Mama Samia kama ni Rais aliyeimarisha urafiki wa kimataifa na sasa wawekezaji wamekuwa wakimiminika, pia kuifanya nchi kung'aa na kuwa kioo kwa nchi zingine nje ya nchi.

**Naogopa-Marioo ft Harmonize**

Ngoma hii ameitoa Aprili 30 mwaka huu inaitwa 'Naogopa', ikitolewa na msanii Marioo, akiwa amemshirikisha 'Tembo', Harmonize.

Ndani ya pini hiyo, jamaa anasema hata akishindia kelele na baba mwenye nyumba apige kelele, hata akipanda daladala ni poa tu, ili mradi asimkose huyo ampendaye.

Kifupi ni kwamba jamaa anakubali shida zote apate, lakini si kumkosa mpenzi wake huyo alinaye. Anachoogopa ataishije bila yeye na si shida zingine za dunia.

**Mdomo-Harmonize ft Ibrah**

Hii sasa ni ngoma ya 'Tembo' mwenyewe, lakini naye akiwa amemshirikisha Ibrah. Ameiita 'Mdomo'. "Waupaka upepo, wanakesha tuachane, tuzikane kesho tukutane kwenye pepo, siyo kulala Buza ushinde Mbezi." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye pini hiyo, iliyoachiwa mwezi uliopita, Aprili 12.

**Killy-Vumilia**


Mmoja kati ya wasanii wanaokuja juu sana, Killy, yeye ametoa ngoma aliyoiita 'Vumilia', akiiachia pia mwezi uliopita, Aprili 16.

Jamaa analalamika mpenzi wake kumtangaza vibaya mitaani. Mpenzi wake friji haligandishi.

"Unatangaza kote hata kitanda si cha kwangu."Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye ngoma hiyo. Hiki ni kisa cha mwanamke asiyemthamini mwanaume. Anayedanganyika na ulimwengu.

**Ibrah-Rara**

Huu ndiyo wimbo uliotoka mapema zaidi mwezi Aprili. Uliachiwa Aprili Mosi. Ni moja kati ya nyimbo ambazo zimeondokewa kupendwa sana kwa sasa sehemu mbalimbali, majumbani, mitaani na kwenye majumba ya starehe.





# Nini kimempata Genevieve Nnaji?

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Genevieve Nnaji amefuta picha zote katika ukurasa wake wa Instagram, hata hivyo hakuna sababu aliyoitoa kutokana na hatua yake hiyo.

Katika jambo la kushangaza, awali Nnaji aliwafuta wafuasi wake milioni nane wanaomfuatilia kila siku na kusababisha watu kuwa na wasiwasi.

Nyota huyo kabla ya kuchukua hatua hizo, mara kadhaa amekuwa akiandika maneno yanayotokana na kitabu kitukufu cha Quran na kuibua minong'ono kwamba huenda amebadili dini.



## May azidi kumbana mumewe

MKE wa kwanza wa mwigizaji mkongwe kutoka Nollywood Yul Edochie, hatimaye amevunja ukimya baada ya mumewe kuchukua mke wa pili.

May ambaye ni mama wa watoto wanne, aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram kwa kuwashukuru kila mtu kwa kumpa moyo baada ya habari ya kushtua kuhusu mume wake kuwa na mke wa pili kuenea kwenye Mtandao.

"Nataka kwa dhati kuthamini kila mtu kwa upendo mkubwa, maombi na usaidizi kutoka kote ulimwenguni. Imekuwa ya kustaajabisha sana. Nyote mmekuwa nguzo ya ajabu katika kipindi hiki cha majaribu," ameandika.

## Sabrina huyoo Kenya

SABRINA Elba, ambaye ni mke wa nyota wa filamu kutoka Hollywood, nchini Marekani amesafiri kwenda Kenya kwa ajili ya shughuli zake za kikazi.

Mrembo huyo ni mwanamitindo wa kimataifa, mwigizaji, balozi wa heshima wa UN na mfuko wa kimataifa wa maendeleo ya kilimo (IFAD).

Kulingana na taarifa kutoka IFAD, Sabrina atakutana na wakulima ambao wanasaidiwa na taasisi hiyo katika maeneo ya Embu na Nyeri.





## Nick, Priyanka warudi nyumbani

MWANAMUZIKI wa Marekani, Nick Jonas na mkewe ambaye ni mwigizaji nyota wa Bollywood, Priyanka Chopra, wamerudi nyumbani baada ya mtoto wao kulazwa miezi mitatu katika chumba cha uangalizi maalum cha ICU.

Wawili hao walitoa taarifa ya pamoja kupitia akaunti ya Instagram kwamba wamerudi nyumbani baada ya kuwa na mtoto wao hospitali wakipigania maisha yake.

"Katika siku hii ya mama duniani inaakisi kile kinachotutokea katika miezi michache, tunajua watu wengi wana uzoefu wa haya tunayopitia. Baada ya siku 100 tukiwa ICU hatimaye binti yetu amerudi nyumbani," ameandika.

## Juliet hayo si mapenzi ni ushetani

MWIGIZAJI mkongwe wa kike kutoka Nollywood, Juliet Ibrahim, amefichua siri kuwa aliwahi kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanaume mmoja ambaye anahisi alikuwa akimbaka.

Amesema kutokana na kile kinachoendelea wakiwa faragha, ilikuwa kama vita kiasi ambacho hakujua kama wapo katika furaha au majonzi.

Mama huyo wa mtoto mmoja, alisimulia kisa hicho alipozungumza kwenye kipindi cha TV cha 'With Chude'. "Ilibidi niachane na uhusiano huo, ilibidi niachane naye. Nilipigania kujiondoa katika uhusiano huo kwa sababu ilifikia hatua alinifungia ndani ya nyumba," amefichua.



# TALGWU: Rais Samia amefuta machozi yaliyodumu miaka 6




Rais Samia Suluhu Hassan akiungana na viongozi wengine kuimba wimbo wa mshikamano wakati wa maadhimisho ya Mei Day yaliyofanyika kitaifa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Mei Mosi, 2022.

**Na Mary Geofrey**

BAADA ya serikali kutangaza nia ya kuongeza mishahara kwa wafanyakazi, Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU), kimeeleza furaha yake na kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwakumbuka baada ya miaka kadhaa kupita.

Katibu Mkuu wa TALGWU, Rashid Mtima, anasema chama hicho kinaungana na wafanyakazi wa kada mbalimbali kuonyesha shukrani zao kwa rais kutangaza neema mwaka ambao chama hicho ndicho kimeratibu sherehe hizo.

Anasema Rais Samia, amejenga ari ya kufanya kazi na kuleta matumaini mapya kwa wafanyakazi ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakisahaulika.

"TALGWU tuna furaha kuandaa sherehe za Mei Mosi kitaifa na Rais ambaye alikuwa mgeni rasmi kutoa ahadi ambayo wengi tulipenda kusikia," anasema Mtima.

Anasema furaha kubwa kwa wafanyakazi ni kuona mkuu wa nchi anatambua na kuthamini kazi kubwa wanayofanya wafanyakazi katika sekta mbalimbali kuleta maendeleo katika Taifa.

"Mtima natoa shukrani kwa niaba ya watumishi wote nchini kwa kuwahakikishia nyongeza ya mishahara. Ni muda mrefu sasa watumishi wa umma hawajapandishiwa mishahara kwani kilio hiki kilikuwa cha muda mrefu na sasa jambo hili linaenda kutekelezwa kama alivyosema Rais Samia,"anaongeza kusema.

TALGWU inaunganisha wafanyakazi wote waliopo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine nchini.

Chama hicho ni miongoni mwa vyama vya wafanyakazi nchini ambacho jukumu lake kuu ni kujenga nguvu ya pamoja ya kutetea haki na maslahi ya wafanyakazi waliopo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa TUCTA, Cornel Magembe, anasema kwa ahadi ya Rais Samia ni wazi kuwa amekubali kuongeza mishahara na anaimani kuwa mwaka wa fedha wa Serikali utakapoanza kutakuwapo na mabadiliko.**



Katibu Mkuu TALGWU Bw.Richard Mtima akizungumza na Waandishi wa habari (hawapo pichani) wakati akito tamko la chama hicho juu ya ahadi zilizotolewa na rais Samia Suluhu Hassan wakati katika maadhimisho ya siku ya Wafanyakazi dunia yaliyofanyika Jijini Dodoma hivi karibuni.

Katika muungano wake ni moja ya vyama vinavyounda Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi vinavyotoa Huduma kwa Umma duniani (PSI) na Mtandao wa Vyama vya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Afrika (AMALGUN).

Katika utendaji wake wa kazi, TALGWU ina jukumu la kuelimisha, kunatetea, na kulinda ajira na ujira wa wanachama wake kwa kuzingatia sheria, taratibu, kanuni, miongozo na nyaraka mbalimbali za kazi.

Katika kuadhimisha sherehe ya Mei Mosi mwaka huu, yenye kauli mbiu isemayo, 'Mishahara na Maslahi Bora kwa Wafanyakazi ndio kilio chetu Kazi Iendelee', inajivunia kwa kuwa na matokeo chanya baada ya miaka sita bila matokeo ya nyongeza za mishahara.

Hali mbaya kwa wafanyakazi inatokana na kukaa miaka mingi bila kuongezwa mshahara, sekta binafsi inafikia miaka tisa.

Katibu huyo anasema wafanyakazi ni injini ya maendeleo katika taifa lolote duniani, hivyo ni vema mchango wao unapaswa utambulike na kuthaminiwa ili kuhakikisha wanaongeza ukuaji wa uchumi wa nchi.

Pia anamshukuru Rais Samia kwa kusikiliza kilio chao kuhusu maslahi ya watumishi walioondolewa kazini kwa vyeti vya kughushi.

"Kama chama kupitia TUCTA kwa muda mrefu tulikuwa tukiiomba serikali kuliangalia kundi hili la Watanzania ambao walitumikia kwa uadilifu nchi yetu,"anasema Mtima.

Anasema Rais Samia ameonyesha upendo mkubwa kwa Watanzania ambao waliitumikia nchi kwa nguvu zao zote hatimaye ameagiza Wizara ya Fedha na mipango kushughulikia na kuwalipa stahiki zao zinazotokana na makato ya mishahara yao.

Mtima anasema agizo kwa mifuko ya hifadhi ya jamii na maofisa utumishi kuhakikisha wanashughulikia haki na stahiki za watumishi wanaotarajiwa kustaafu linazidi kuwapa faraja zaidi.

Anasema kuundwa kwa bodi ya kima cha chini cha mishahara kwa sekta ya umma ambayo imeshaanza kufanya kuthmini ya mishahara ni jambo kubwa na la kuigwa na viongozi wengine.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa TUCTA, Cornel Magembe, anasema kwa ahadi ya Rais Samia ni wazi kuwa amekubali kuongeza mishahara na anaimani kuwa mwaka wa fedha wa Serikali utakapoanza kutakuwapo na mabadiliko.

Anawaomba wafanyakazi kuwa na subira katika kipindi hiki kwa sababu kiongozi huyo wa nchi hajawahi kusema na kutotekeleza,

"Rais ni kiongozi mkubwa hawezi kwenda kinyume hivyo niwaombe wafanyakazi wavute subira kwani mwaka wa fedha wa serikali unaanza mwezi wa saba na ninaimani kipo kitu kitaongezeka," anasisitiza.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAPOKWENDA...

# Michezo, nyimbo za watoto enzi hizo

## •Nyingi zimerudiwa na wanamuziki
## •Za kurukia kamba nazo zimo

Na Adam Fungamwango



ULIKUWA ni wakati wa watoto kucheza pamoja. Ulikuwa ni wakati wa watoto ambao walikuwa wakifahamiana mtaa mzima. Hata kama wazazi hawafahamiani, lakini watafahamiana na kuunda ujirani na urafiki kwa sababu ya watoto.

Ni wakati ambao mijini watu walikuwa hawajaanza kujenga nyumba na kuzungushia uzio wa ukuta na mageti. Ukiona uzio basi utakuwa ni wa nyasi, makuti, au miti ya michongoma. Inawezekana vijijini maisha kama haya bado yapo, ingawa aina hii ya maisha inaanza kufutika taratibu.

Mijini, imebaki kubwa historia. Nakumbuka miaka ya 1990 kurudi nyuma, kipindi watoto wamerudi mashuleni, hasa ikifika saa 12:00 jioni, watoto hukusanyika na kuanza michezo mbalimbali, ikiwemo kuimba.

Kulikuwa na michezo ambayo huwezi kuicheza bila kuimba nyimbo. Pia kulikuwa na nyimbo tu ambazo zilikuwa zikiimbwa wakati huo wakisubiri chakula makwao, baadaye kwenda kulala.

Mpaka leo haijajulikana zilikuwa zinatungwa na nani, lakini zilikuwa maarufu sana na zilijulikana na watoto wote Tanzania nzima. Ni nyimbo chache sana ndiyo zilikuwa zinaweza kuwa ni za mkoa fulani, kwingine huwezi kuzisikia.

Nyimbo hizo mwanzoni mwa miaka ya 2000, zilianza kurudiwa na bendi mbalimbali za muziki wa dansi za kizazi kipya kama African Stars 'Twanga Pepeta', Mchinga Sound, TOT Plus, African Revolution 'Tamtam' na hasa kwenye vibwagizo vyao.

Leo tutaziangalia baadhi ya nyimbo za watoto ambazo zilikuwa maarufu sana, zikiimbwa kwa sababu mbalimbali kama vile kwenye michezo na mambo mengine yanayofanana na hayo.

### NYIMBO ZA MICHEZO

Tukianza na nyimbo za michezo, kuna ile ya kurukia kamba. Kuna wimbo mmoja uliopigwa na Juwata Jazz Band uitwao 'Aziza'. Huu ulitumika sana kwenye mchezo huo na kuwa maarufu sana. Sidhani kama wale watoto na wasichana wa zamani ambao kwa sasa watakuwa kinamama watu wazima watashindwa kuufahamu wimbo huu.

"Aziza sasa naomba, turudiane, hayo yamekwisha, kipenzi changu, shetani katupitia, rudi mke wangu ee, mimi mwenzio mama ninapata tabu."

Kuna wimbo mwingine ambao unaitwa 'Shilingi ya Nyerere'. "Shilingi ya Nyerere katikati kuna mwenge, doli doli, doli samwela." Mara nyingi mchezo huu ni kwamba watoto au wasichana wawili wanashika kamba, upande mmoja na mwingine,

**"Bilinge bayoyo bilinge bayoyo, bilinge bayoyo tunamuomba dada Asha uje hapa, kaa chini tukuone maringo yako, bingilibingili mpaka chini." Pia kuwa wimbo wa kinyulinyuli.**

huku anayeruka anakuwa kati. Zile nyimbo ambazo huwa zinaimbwa na wote, mrukaji, walioshika kamba na hata wanaoangalia, huwa ni burudani na kumhamasisha anayeruka ili asikosee. Akikosea anatoka anaingia mwingine.

"Kioo kioo, alikivunja nani, sijui sijui, waongo nyie wote, piteni piteni, wa mwisho akamatwe, atiwe gerezani."

Huu ni wimbo uliokuwa unatumika kwenye mchezo wa kioo. Hauna jinsia, kwani ulichezwa na wote, wavulana na wasichana.

Wawili wanashikana mikono wakiwa wameiinua juu, na watoto wengine wanapita kwa foleni katikati ya wawili walioshikana mikoni, lakini wakiwa chini ya ile mikono yao iliyoshikana kwa juu.

Mwisho wa wimbo, wanaishusha chini na kumbana yule ambaye wimbo umemalizika akiwa katikati yao na juu ya mikono.

"Namsaka mke wangu namsaka mke wangu, hapa hayupo hapa hayupo, kaenda wapi kaenda wapi, kaenda kusuka kaenda kusuka, kitana kampa nani, kitana kampa nani? Kampa msusi kampa msusi, kioo kampa nani kioo kampa nani? Kampa msusi kampa msusi." Huu ni moja wa wimbo maarufu wenye michezo ya kitoto ambao maneno yake yaliwekwa kwenye wimbo mmoja wa TOT Plus.



"Yai bovu yai bovu, linanuka linanuka, linanukaje linanukaje? Pwi pwi pwi. Nina ndoo yangu, ya kuchota maji, maji ya barafu, watoto masitizame nyuma, yai bovu linapita." Wimbo huu huimbwa kwenye mchezo huo ambao watoto wanakuwa wamekaa chini na kutengeneza mduara mkubwa. Anayeimbisha ndiye anayekuwa anazunguka na kitu au kitambaaa kilichofinyangwa kama mpira hivi. Hilo ndiyo yai bovu lenyewe. Halafu akishasema msitizame nyuma, ule mpira anauweka nyuma ya mtu yoyote aliyekaa ambaye yeye amemchagua. Atayewekewa atasimama na ule mpira na kumpiga nao aliyeimbisha. Kama ukimpata, basi aliyeimbisha atarudia tena kuimbisha, lakini kama ukimkosa, yule aliyewekewa lile tambara la yai bovu, basi ataanza kuimbisha yeye.

### NYIMBO ZILIZORUDIWA NA BENDI

Kuna nyimbo nyingi za watoto enzi zile ambazo miaka ya 2000 maneno yake yalirudiwa na baadhi ya bendi katika kunogesha vionjo, na kuwakumbusha watu mbali.

"Amina, Amina kadala, (snowea), Amina dumpepe dumpepe, Amina Magereza, Amoina dush dush. Dada kama wanipenda, kaninunulie zeze, nikilala kitandani, zeze lanibembeleza, dada Maida, kuchomachoma kubaya, utamchoma mkweo, aliyekuzalia mumeo." Baada ya hapo kuna mwingine unaimbwa

"Bilinge bayoyo bilinge bayoyo, bilinge bayoyo tunamuomba dada Asha uje hapa, kaa chini tukuone maringo yako, bingilibingili mpaka chini." Pia kuwa wimbo wa kinyulinyuli.

"Kinyulinyuli nyulika mwanangwa wa Jumbe, kavaa nguo mbili, ya tatu kajifunika."

Mbali na hizo kuna zingine kama

"Moja chama chetu cha umoja, mbili macho kama pilipili, tatu, ratu mwizi wa mapera, Mwanne acha uhuni, tano, kwa mchuzi wa manjano, sita, baharini kuna vita, saba, sabasaba imefika, nane, zunguka tuonane, tisa, kwa Mzungu kunatisha, kumi, kwa mateke na mangumi."

Upo pia wa mkulima mwenye shamba.

"Mkulima mwenye shamba alipanda viazi, akachimbachimba akaona mali, lololo bahati ya mtu mwenye shamba, akatupa jembe upande akaenda mjini, kununua moto kali sasa ni tajiri, lololo bahati ya mtu mwenye shamba."

**Tuma meseji 0716 350534**

## Mkenya ashinda tuzo ya muuguzi bora Duniani

**NAIROBI,** KENYA

MUUGUZI kutoka Kenya ameshinda tuzo ya kwanza ya uuguzi Duniani ambayo ina zawadi ya Dola 250,000.

Anna Qabale Duba, ambaye anafanya kazi katika Hospitali ya Rufaa ya Kaunti ya Marsabit, kaskazini mwa Kenya, alitunukiwa tuzo hiyo kwa kujitolea kutokomeza mila potofu kama vile ya ukeketaji katika jamii yake.

Duba pia ameanzisha taasisi yake inayoitwa Qabale Duba Foundation inayolenga kuwawezesha wasichana wadogo.

"Kupitia shirika langu, nimejenga shule ya kipekee kijijini kwangu inayofundisha watoto na wazazi wao, kwa sababu kwangu elimu ni muhimu kwa maisha bora ya baadaye," alisema Duba.

Zaidi ya wauguzi 24,000 kutoka nchi 184 waliwasilisha maombi yao.

## Mwanafunzi auawa kwa kukashifu uislam

**Abuja,** NIGERIA

Mwanafunzi wa Nigeria auawa kufuatia madai ya kukashifu uislamu

Ghasia zimezuka katika chuo cha elimu ya juu katika mji wa Sokoto kaskazini mwa Nigeria baada ya mwanafunzi wa kike wa Kikristo kudaiwa kutoa matamshi ya kashfa dhidi ya Uislamu.

Wanafunzi wa Kiislamu katika Chuo cha Elimu cha Shehu Shagari, wanaripotiwa kumuua msichana huyo na kuuchoma moto mwili wake.

Kisha waliingia kwenye msako wa kuharibu mali kadhaa yakiwemo magari.

Msemaji wa Polisi katika jimbo la Sokoto, aliambia BBC kuwa vikosi vya usalama viliingilia kati kurejesha hali ya utulivu na uchunguzi unaendelea.

Mamlaka imekifunga chuo hicho kwa muda usiojulikana na kuwaamuru wanafunzi kurudi nyumbani mara moja.

Kiongozi mkuu wa kidini wa Kiislamu nchini Nigeria, Sultan wa Sokoto, Sa'ad Abubakar, amelaani mauaji ya mwanafunzi huyo wa Kikristo na kuomba utulivu.

# Russia yatoa onyo kali kwa Finland, yaapa kulipiza kisasi kisichotarajiwa

**MOSCOW,** RUSSIA

RUSSIA imeonya kwamba italazimika kuchukua hatua za kulipiza kisasi kutokana na hatua ya Finland kujiunga na Nato.

Taarifa ya wizara ya mambo ya nje ya Russia, ilisema jana kuwa hatua hiyo itaharibu sehemu kubwa ya uhusiano wa nchi hizo mbili, pamoja na usalama na uthabiti kaskazini mwa Ulaya.

Awali, Rais na Waziri Mkuu wa Finland, walitoa wito kwa nchi hiyo kuomba uanachama wa Nato bila kuchelewa.

Kauli hiyo inakuja huku kukiwa na ongezeko la uungwaji mkono wa umma kwa wanachama wa Nato kufuatia uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

Finland inapakana na Russia mpaka wenye urefu wa kilomita 1,300 sawa na maili 81. Hata hivyo hadi sasa imebaki nje ya Nato ili kuzuia kuchukiza jirani yake wa mashariki.

Finland itatangaza rasmi uamuzi wake kesho baada ya kupitishwa na bunge na viongozi wengine wakuu wa kisiasa.

Sweden ilisema itatangaza uamuzi kama huo siku hiyo hiyo.

Katibu Mkuu wa Nato Jens Stoltenberg alisema anatarajia mchakato wa kuipa Sweden na Finland uanachama haraka.

Mbunge achelewesha msaada kwenda Ukraine

Marekani imekuwa na jitihada za kutuma haraka msaada wa Dola bilioni 40 kwa ajili ya kusaidia Ukraine.

Wabunge wa Seneti kutoka vyama vya Democrats na Republican, waliungana kama ishara ya nadra ya umoja kwani wote walikubaliana juu ya hitaji la kutuma haraka msaada mkubwa zaidi katika miongo kadhaa.

Lakini seneta mmoja, Rand Paul wa Republican kutoka Kentucky, alijaribu kuchelewesha muswaada huo.

Paul, ambaye kihistoria amepinga matumizi ya fedha katika misaada ya kigeni, alikataa kuunga mkono pendekezo hilo ambalo lilihitaji kuungwa mkono kwa kauli moja.

Anadai sheria ibadilishwe ili kumtaka ofisa kusimamia matumizi katika mzozo huo.

"Ikiwa Seneta Paul ataendelea na madai yake... atafanikiwa kuchelewesha msaada unaohitajika sana Ukraine," Kiongozi wa wabunge wengi, Chuck Schumer alisema.

UK- Putin anajidhalilisha mbele ya Dunia

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza, Liz Truss, amesema vikwazo vya kimataifa dhidi ya Russia vinapaswa kuondolewa pale wanajeshi wote wameondoka nchini Ukraine.

Liz aliuambia mkutano wa mawaziri wa mambo ya nje wa G7 nchini Ujerumani, kuwa Rais Vladimir Putin lazima akabiliane na kushindwa jambo litakalozuia uchokozi.

"Putin anajidhalilisha katika jukwaa la dunia, lazima anyimwe manufaa yoyote kutokana na uvamizi wake nchini Ukraine," alisema.

Pia alitoa wito kuongeza upatikanaji wa zana za kijeshi za Nato nchini Ukraine.




Gari likipita pembeni ya roketi iliyorushwa na Russia na kuangukia katika barabara karibu na kijiji cha Kuhari, Kaskazini magharibi mwa mji wa Kyiv nchini Ukraine jana: **PICHA: THE NEW YORK TIMES**

# Afrika Kusini yataka chanjo za Covid-19 kununuliwa zinazotengenezwa Afrika

**CAPETOWN,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa ameyataka mashirika ya kimataifa na wafadhili kununua chanjo za Covid-19 kutoka kwa wazalishaji wa Kiafrika.

Ramaphosa alisema hatua hiyo itahakikisha uwezo unaoendelea katika bara hilo unadumishwa.

Kiongozi huyo alizungumza hayo katika mkutano wa kilele wa kimataifa kuhusu ugonjwa wa Covid 19 siku ya Alhamisi.

"Mashirika ya kimataifa ambayo yamechangiwa fedha nyingi kwa ajili ya kununua na kupata chanjo kwa nchi zinazoendelea kiuchumi, hayanunui chanjo kutoka kwa watengenezaji ndani ya bara la Afrika, hata kwa zile chanjo ambazo zimewekwa kwa nchi za Afrika," alisema.

Kauli hiyo inakuja wakati mtengenezaji wa chanjo nchini Afrika Kusini, alitoa angalizo la kusimamisha uzalishaji wa chanjo kwa kukosa watu wanaoagiza.

Kampuni ya Aspen Pharmacare hivi karibuni ilisema inaweza kulazimika kusitisha uzalishaji katika kiwanda chake cha Afrika Kusini baada ya kukumbwa na uhitaji mdogo.

Kampuni ilijadili mkataba wa kutoa leseni mwezi Novemba ili kufunga na kuuza chanjo ya Johnson & Johnson ili kusambazwa barani Afrika.

Kati ya Waafrika sita, mmoja ndio amepata dozi mbili za chanjo ya virusi vya corona, huku wengi wakisita kuchanjwa.

**Habari zote na BBC**

# TFWG kutoa elimu ya kuhifadhi misitu

Na Christina Haule, MOROGORO

JUKWAA la vyama vya kiraia na watu binafsi wanaofanya kazi za kuboresha misitu kwa manufaa Tanzania (TFWG) limejipanga kutoa elimu za kuhifadhi misitu kwa jamii kwa kuzingatia usawa wa kijinsia ili kuleta tija na ushiriki wa uhifadhi kwa jamii yote kwa ujumla.

Mmoja wa wadau wa jukwaa hilo, ofisa wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Simon Lugazo, alisema jana kwenye warsha ya kuwajengea uwezo wadau wa jukwaa hilo mjini hapa kuwa elimu ya masuala ya usawa wa kijinsia inapaswa kutolewa kwa jamii ikiwajumuisha wazee na vijana.

Alisema kuwa makundi hayo yakishapata elimu hiyo, kwa pamoja yatatambua na kunufaika na shughuli za usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii (USMJ) zinazopaswa kufanywa ili kulinda mazingira.

Lugazo alisema ni vyema kuingiza masuala ya jinsia kwenye sera za ndani za vijiji jambo litakalosadia jamii kwa ujumla kuona manufaa ya kushiriki USMJ kupitia jukwaa la TFWG ikiwamo mradi wa mkaa endelevu.

Mtafiti wa Masuala ya Jinsia kutoa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Emmanuel Mroto, alisema katika tafiti zilizofanywa tangu mwaka 2015 kwenye Wilaya za Mvomero, Kilosa na Morogoro wamebaini kuwa tangu TFCG walipoanzisha mradi wa mkaa endelevu, mitazamo ya kijinsia imebadilika na wanawake wanajikita kwenye shughuli za kuhifadhi misitu hasa kusomba miti midogo na kusogeza kwenye tanuru la kuchoma mkaa na kutoa mkaa na kusafirisha kibiashara mikoani.

Meneja Misitu na Mradi wa Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC), Alex Njahani, alisema wamekuwa wakigusa makundi yote ya kijamii kwenye miradi wanayofanya katika kongani zao mbalimbali za misitu zilizoko kwenye mikoa ya Ruvuma, Tanga na Lindi na kuleta tija katika mazao ya asali, uyoga, mbao na mkaa ili kuboresha shughuli za uhifadhi wa misitu nchini.

Mwezeshaji wa warsha hiyo, Deogratius Mfugale, alisema linapokuja suala la mwanamke kumiliki rasilimali, jamii inapaswa itambue kuwa nao wana haki sawa kama wanaume na wanapaswa kunufaika.

Akizungumza kwenye warsha hiyo, Ofisa Msaidizi wa mradi kutoka Jumuiko la Maliasili Tanzania, Fadhila Kaleta, alisema amenufaika na warsha hiyo kwa kujua kuwa mwanamke ana uwezo wa kufanya kazi ambazo mwanaume anazifanya kwenye shughuli za kuhifadhi misitu na hivyo watamwingiza katika nafasi zote.

TFWG hufanya kazi kuboresha misitu kwa ajili ya uhifadhi na kuhakikisha wadau wote wananufaika, ikiwamo jamii na serikali kuu ambapo mpaka sasa ina washiriki 19 wakiwamo MJUMITA, JET, TFCG, WWF.

# Wizi wa ng'ombe wampeleka jela

Na Joctan Ngelly, GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imemhukumu Luhamy Sembe (32) kutumikia kifungo cha miaka saba jela kwa kosa la wizi wa ng'ombe 35 wenye thamani ya Sh. milioni 23, mali ya Robert Jonathani.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Cleofas Waane, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasi na kuacha shaka.

Hakimu Waane alisema mahakama hiyo inatoa adhabu hiyo dhidi ya mshtakiwa ili liwe fundisho kwake na vijana wengine wenye tabia ya wizi kama yake.

Katika kesi hiyo, upande wa mashtaka ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Monica Matwe, aliyepeleka mahakamani huko mashahidi watano na vielelezo vinne ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Katika hati ya mashtaka, ilidaiwa kuwa Januari 27, 2021, akiwa Kijiji cha Nyamwilolelwa Mkoa wa Geita, mshtakiwa huyo aliiba ng'ombe 35 waliokuwa kwenye zizi na kukimbia na kutokomea kusikojulikana.

Wakili huyo alidai kuwa baada ya ng'ombe hao kuibwa, mlalamikaji alikwenda kutoa taarifa polisi na baada ya muda alipewa taarifa na askari polisi wa Masumbwe Wilaya ya Mbogwe kuwa kuna ng'ombe wamekamatwa kwenye mnada wa Masumbwe na kutakiwa kwenda kuwaona na alipofika mnadani alikuta ng'ombe hao ni wake.

Alidai askari polisi waliwakamata ng'ombe hao pamoja na mshtakiwa huyo na walipofika Kituo cha Polisi Geita, mshtakiwa alipohojiwa kuhusiana na wizi huo, alikiri kuiba ng'ombe hao na baada ya mahojiano hayo, alifikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Hakimu Waane alisema ameangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote na mshtakiwa umetiwa hatiani kwa kosa aliloshtakiwa nalo.

Mshtakiwa alipopewa nafasi ya kujitetea kabla ya kupewa adhabu, aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa mke wake ana ujauzito wa miezi minne, bibi yake na watoto wanne wanamtegemea.

Wakili wa Serikali, Monica, aliomba mahakama hiyo itoe adhabu kwa mujibu wa sheria ili kupunguza wimbi la wizi wa mifugo katika Mkoa wa Geita.

Hakimu Waane alitupilia mbali utetezi wa mshtakiwa huyo na kusema mshtakiwa utakwenda kutumikia kifungo cha miaka saba jela na upande ambao haujaridhika na hukumu hiyo, rufani iko wazi.



Wafanyabiashara wadogo wakiwa wamepanga bidhaa zao katika eneo la kusimama abiria wanaposubiri usafiri katika kituo cha mabasi cha Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam juzi na kusababisha usumbufu mkubwa. **PICHA: SABATO KASIKA**

# PURA yajizatiti mradi gesi asilia

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) imesema imejipanga kikamilifu kusimamia Mradi wa Kubadili Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) ili ulete tija na kuchangia maendeleo ya uchumi.

Mjiolojia Fortunatus Kidayi aliyasema hayo jana wakati akitoa maelezo kwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack, alipotembelea banda la PURA katika maonyesho ya tano ya mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi yanayoendelea mkoani Morogoro.

Alisema miongoni mwa majukumu ya PURA kwa mujibu wa Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 ni kusimamia mradi wa LNG.

Alisema mradi huo unalenga kuvuna gesi asilia iliyogunduliwa kina kirefu cha Bahari ya Hindi kwa ajili ya matumizi ya ndani na kiasi kingine kuuzwa nje ya nchi.

"Mradi huu ni wa thamani ya Dola za Marekani bilioni 30 na unatarajiwa kutekelezwa eneo la Likong'o mkoani Lindi, PURA imeendelea kujiimarisha kiutendaji ikiwamo kuendelea kuwajengea watumishi wake uwezo katika eneo la LNG," alibainisha

Kidayi alisema wamejipanga kuhakikisha Watanzania wanapata fursa ya kushiriki katika mradi wa LNG kupitia ajira na utoaji wa huduma na bidhaa katika kipindi chote cha utekelezaji wake.

"PURA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) tumeandaa kanzidata ya kuwasajili watoa huduma wazawa wenye taaluma mbalimbali ikiwamo masuala ya mafuta na gesi. Kanzidata hii inajulikana kwa jina la Common Qualification System (CQS) na iko tayari kutumika," alisema.

Aliongeza mradi wa LNG unatarajiwa kuleta fursa nyingi ikiwa ni pamoja na ajira zaidi 6,000 na za kuuza bidhaa na huduma wakati wa utekelezaji wa mradi huo.

"Serikali ilishatoa Sh. bilioni 5.7 kulipa fidia kwa wananchi zaidi ya 640 waliopisha utekelezaji wa mradi, majadiliano baina ya Serikali na kampuni zitakazotekeleza mradi wa LNG yanaendelea na yanatarajiwa kukamilika hivi karibuni," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Telack alisema wananchi mkoani humo wanasubiri kwa hamu kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo na kwamba ana imani watapewa kipaumbele wakati wa utekelezaji wake.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-5

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Hawakuongea chochote hadi walipofika nyumbani. Alimuachia mkono na kufungua mlango. Akamshika tena mkono na kumuingiza ndani. Bado alionekana amekasirika.

"Yaani wameniboa wale. Watu gani hawana hata huruma." Alilalamika. "Bakari utakaa hapa, utaishi hapa siyo mwezi mmoja, muda wowote unaoona kuwa utafaa wewe kuondoka, iwe mwezi, miezi miwili, mitatu sawa tu."

"Sasa huyo mwenyekiti si hataki, anaweza kukukamata..."

"Siyo kazi yako, hiyo niachie mimi, kama kupewa adhabu, kukamatwa, kuchinjwa, niachie mimi ndiye nitakayejua hilo." Alijibu akionekana bado ana hasira.

Taarifa za Siwatu kumhifadhi mtu aliyeokotwa majeruhi kwenye kijiji hicho zilifika kwa Mwenyekiti wa Kijiji.

Yeye alitaka aondoke baada ya siku tatu. Hakutaka kutoa adhabu yoyote kutokana na historia ya binti mwenyewe. Ni yatima na jinsi alivyoondokewa na wazazi wake, kila mtu anajua na wengi wamekuwa wakimuonea huruma. Licha ya yote hayo, hakuwa binti mwenye mambo mengi. Alikuwa na akili, nidhamu na adabu, hivyo alihofia kufanya maamuzi ya peke yake.

Akaitisha kikao cha kijiji kumjadili. Kumjadili Siwatu aliyekiuka sheria, kanuni na utamaduni uliowekwa na kijiji hicho cha Semwanza.

*************************

"Wanajijiji nimewaiteni hapa kuelezea tukio lililotokea hapa kijijini kwetu. Siku hizi mbili tatu, tulipokea mgeni, ambaye hakujulikana ametoka wapi. Baadaye tukaja kujua kuwa ametokea Msata. Mgeni huyu alikutwa amejeruhiwa vibaya kule karibu na barabara kuu. Mwenyewe anasema alijeruhiwa na watu wa kwao huko Msata, walimpiga na kuja kumtupa pale.

Ameshatibiwa, lakini hataki kuondoka. Na kibaya zaidi mwanakijiji mwenzetu Siwatu ndiye anayemkingia kifua." Ilikuwa sauti ya Mwenyekiti wa Kijiji, mzee Hassan.

Maneno hayo yalizua vicheko na maneno ya chinichini kutoka kwa kinadada na kinamama.

"Keshajipatia mchumba huyo." Ilisikika sauti ya kike.

"Sasa hata kama mchumba, kuna




**"Siyo kazi yako, hiyo niachie mimi, kama kupewa adhabu, kukamatwa, kuchinjwa, niachie mimi ndiye nitakayejua hilo." Alijibu akionekana bado ana hasira.**

utaratibu wake. Kinachotakiwa ni kwamba yule kijana aende kwao, akaongee na mshenga, aje hapa, alete barua, na mambo ya posa yafanyike na baadaye harusi, sasa kama bwana anataka kukaa hapa sawa, amchukue sawa, lakini hii si sahihi. Unajua tunaweza tukawa tunakaa na mtu, lakini kumbe amekuja hapa ana nia mbaya. Labda jasusi, kuna kitu anapeleleza kwenye kijiji chetu, au lengo lake hapa ni baya kwa kijiji au mwanakijiji mmoja mmoja." Baadhi ya wanakijiji walipiga makofi.

Mwenyekiti alimwita mmoja wa mwanakijiji aliyenyoosha kidole aje mbele.

"Mwenyekiti na wanakijiji mwenzangu, mimi napendekeza kitu kimoja, Siwatu na huyo mgeni wake watimuliwe kijijini."Ni sauti iliyofuatiwa na kelele, mayowe na makofi, ikionekana wengi wanaunga mkono jambo hilo, ingawa baadhi walikaa kimya. Hawakuonekana kuunga mkono.

"Tunashukuru mwanakijiji kwa ushauri wako. Mimi mwenyewe nilitaka kutoa uamuzi kama huo, lakini kwenye kijiji huwa kuna wazee. Wazee ni tunu kwenye taifa lolote, na hata kijiji chochote. Nilikaa nao, nikawaeleza, lakini wao walikataa suala la kumfukuza Siwatu kijijini.

"Afukuzwe bwana, huyu msichana tumemdekeza wenyewe. Hebu angalia hata kwenye mkutano hajaja, yeye na huyo hawara yake." Dada mmoja alidakia na kusababisha vicheko kutoka kwa wenzake.

Mwenyekiti naye ilibidi aangue kicheko, halafu akaendelea kuongea.

"Ni kweli, lakini wazee waliniambia kuwa pamoja na yote aliyoyafanya, lakini hapaswi kufukuzwa. Bado ni mwanakijiji mwezetu na hajafanya jambo baya kihivyo. Hajaua mtu. Ingawa kumhifadhi mtu ambaye hajulikani sawasawa alikotoka ni tatizo, kitu ambacho walichoamua ni kumtenga.

Wamesema akitengwa, yeye na mwenzake, basi wao wenyewe wanaweza wakaamua cha kufanya. Makali ya kutengwa yanaweza kusababisha mgeni aondoke, au waondoke wote, tukumbuke kuwa Siwatu ni mtoto yatima, msichana ambaye wote tunajua historia yake, alifiwa na wazazi wake akiwa bado mdogo, tumemlea wenyewe. Yaani amelelewa na wanakijiji, na kama tunavyofahamu ana kaupendeleo maalum kutokana na historia yake ya kusikitisha, ndiyo maana wazee wameamua kutokwenda mbali zaidi na hapo, kwa sababu baya lolote litakalomfika, mizimu ya wazazi wake na ya kijiji hiki haitotuacha salama." Mkutano sasa ukawa kimya. Zilibaki sauti za kunong'ona tu. Inavyoonekana ni kwamba somo lilianza kuwaingia wanakijiji.

"Wameamua kuwa asiuziwe kitu chochote dukani, au kushirikiana naye kwa shughuli zozote za kijamii hadi hapo atakapofanya mambo ambayo tumemuelekeza. Amuondoe kwanza mgeni wake. Tunajua na tunamsifu kuwa yeye ndiye aliyesababisha aokolewe, kibinadamu anastahili sifa, lakini kiusalama wa kijiji chetu, alitakiwa aondoke kwanza. Na kama anataka kuwa mwanakijiji kuna vitu vya kufanya ili akubaliwe, tujue ametoka wapi, kwa nini anataka kukaa hapa, huko alikotoka alitoka kwa usalama? Ni mtu mwema? na mengine mengi, lakini hili halijatimizwa. Kitu pekee ambacho wazee wa kijiji wameamua asizuiliwe ni kwenda shambani kulima na kuchota maji tu. Kwa haya niliyoyasema nafunga mkutano, nadhani wote tumeelewana na vikwazo hivi vinaanza mara moja. Akaambiwe kuwa kijiji kimeamua hivyo." Akamaliza Mwenyekiti Hassan na watu wakaanza kuondoka taratibu, stori zima njiani kila mtu ilikuwa ni Siwatu.

*************************

"Mimi nadhani bora tu kesho niondoke Siwatu."

"Kwa nini?" Akajibu na kumtazama Bakari kwa jicho kali. Mwenyewe aligundua hilo na kuyaondoa macho yake taratibu kwa Siwatu.

"Kwa hayo uliyoniambia kuwa wamekutenga. Mimi nakuonea huruma sana. Ulikuwa umekaa vizuri kijijini, ukawa kipenzi cha kila mtu. Leo wanakutenga kwa ajili yangu. Mtu ambaye nimefika hapa kwa bahati mbaya. Ambaye siwezi kukusaidia wewe kwa chochote. Mtu ambaye ni tegemezi kwako, kwani nimefika hapa nikiwa majeruhi, sina nguo, sina pesa."

"Sijui unaongea nini Bakari. Kwangu mimi ngumu zaidi ilikuwa ni kukusogelea wewe ukiwa umechakaa na sura yako kufunikwa na damu kwa ajili ya kipigo. Nilikuwa sijui wewe ni nani. Ni majeruhi au tayari marehemu. Wenzangu wakaondoka, nikakumwagia maji kwa ajili ya kusafisha damu, ukaonyesha ishara ya kutaka maji ya kunywa, nikakunywesha. Ilikuwa ni jioni, saa 12:00, porini. Pata picha mimi ni mtoto wa kike, nilifanya yote haya, nikijua ninalofanya inawezekana ikawa ni hatari kwa maisha yangu. Leo eti wamenitenga, ndiyo niogope? Kama unataka kwenda nenda, lakini siyo iwe unaondoka kwa sababu yangu." Sauti ilikuwa ndogo, lakini yenye msisitizo iliyojaa kila aina ya ukweli na ushupavu wa kike.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KIFARU ALIA SAFU YA ULINZI MTIBWA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuchapwa mabao 3-2 na KMC, Msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru amesema kuwa safu ya ulinzi imewaangusha, huku akibainisha kuwa wachezaji wao wengi kwenye safu hiyo hawakuwepo kwa sababu mbalimbali.

Akizungumza mara baada ya kupoteza mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania juzi kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, kifaru alisema ni kutokana na kukosekana kwa mabeki mahiri kwenye kikosi hicho kama Abdi Banda, Ibrahim Ame na Oscar Masai.

"Tumepoteza, hatukuwa vizuri hasa kwenye eneo la kujilinda, tumeongoza mchezo muda mwingi, lakini uzembe wa mabeki wetu ndiyo umetugharimu, lakini ndiyo makosa ya kimpira, kwa sababu hatukuwa na mabeki wetu tunaowategemea.

"Banda anauguliwa na mama yake mzazi, Ame yeye alikuwa majeruhi, amepona kwa sasa lakini bado hajawa fiti, na Oscar Masai ambaye alikuwa anatumikia kadi, na pengo lake lilionekana dhahiri, huku Masai ni beki mzuri sana na tegemeo kubwa kwenye safu ya ulinzi ya Mtibwa Sugar kwa sasa," alisema Kifaru.

Hata hivyo alisema kuwa wanakwenda kuiangalia mechi nyingine na si hiyo, kwani Mtibwa Sugar ilipotoka siyo kama ilivyo sasa, natumai tutashinda tu.

"Kwa sasa tumeimarika sana tofauti na tulivyoanza ligi, hata hii mechi tulikuwa tumeshaimaliza, ni sisi wenyewe tu, walikuwa wetu tu wale," alisema.

Mtibwa ambayo hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza ilikuwa inaburuza mkia, kwa sasa inashika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 27, huku KMC ikipanda hadi kwenye nafasi ya tisa, ikiwa na pointi hizo hizo 27.




Bondia wa ngumi za kulipwa Tanzania, Mfaume Mfaume (katikati) akizungumza na waandishi wa habari jana kuelekea pambano lake dhidi ya Abdumonem Said wa Misri la kuwania mkanda wa WBF litakalofanyika Juni 10 mwaka huu, Dar es Salaam. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Coastal haina kulala

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA mkuu wa Klabu ya Coastal Union, Juma Mgunda amesema timu yake imejipanga vizuri kwenye mchezo dhidi ya Mtibwa Sugar utakaopigwa kesho Jumapili huku akiahidi kuondoka na pointi zote tatu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda alisema wachezaji wake wanaendelea vizuri huku wale waliokuwa majeruhi, Musa Athumani, Mtenje Albano pamoja na mlinda mlango Musa Mbisa wameanza kufanya mazoezi mepesi.

"Tumejipanga kupata pointi tatu katika mchezo huo tunafahamu Mtibwa ni timu nzuri ambayo sasa hivi inaimarika kila siku na tunafahamu tunakwenda kukutana na timu ambayo imepoteza mchezo wake uliopita lazima tutaingia kwa tahadhari kubwa," alisema Mgunda.

Alisema baada ya kupata pointi 6 katika michezo miwili iliyopita wanaelekeza akili na nguvu zao katika mchezo huo ambao amekiri utakuwa mgumu. Alisema lengo ni kupata pointi 3 kwenye kila mchezo uliopo mbele yao ili washike nafasi ya juu katika msimamo wa Ligi Kuu.

Aliomba mashabiki wa Klabu hiyo waendelee kuwaunga mkono ili wafanye vizuri katika michezo hiyo licha ya Ligi kuwa na ushindani.

## Bogos Musica waanza na 'Arumbaya'

**Na Sabato Kasika**

RAIS wa bendi ya Bogos Musica, Nyoshi El-Sadat amesema amesambaza wimbo mpya uitwao 'Arumbaya' katika vituo vya redio na televisheni kwa ajili ya kutambulisha ujio wa albamu ya kwanza ya bendi hiyo kwa mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Rais huyo alisema albamu wanayoiandaa itakuwa na nyimbo 12, huku akitaja chache kuwa ni 'Mwisho wa Ubaya, Zena na Nicole'.

"Tunajiandaa kutambulisha 'Arumbaya' katika onyesho la Wafia Dansi litakalofanyika Dar es Salaam mwishoni mwa mwezi huu ili mashabiki wetu wafurahie ujio albamu mpya," alisema Nyoshi.

Nyoshi alisema, bendi yake ni miongoni mwa tano zilizoalikwa kushiriki katika onyesho hilo zikiwamo za Msondo Ngoma Music, Mapacha Music, Mjengoni Classic ya jijini Arusha na Waluguru Orignal ya Morogoro.

Lakini pia tunajiandaa kufanya uzinduzi wa albamu yetu Julai mwaka huu, ndiyo maana tumepeleka wimbo mmoja katika vituo vya redio na televisheni ili kutambulisha ujio wa albamu yetu mpya," alisema.

Nyoshi ambaye pia ni mwimbaji, alisema bendi yake ina wanamuziki 22 huku wengi wakiwa ni vijana ambao anaamini kuwa wanaweza kuifikisha mbali katika mafanikio, kwa madai kwamba wanajituma katika kazi.

## Bondia Mfaume kuwania mkanda wa WBF

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutoonekana ulingoni kwa mwaka mmoja na miezi sita, Bondia wa ngumi za kulipwa nchini, Mfaume Mfaume anarejea kwa mara nyingine dhidi ya Mmisri, Abdumonem Said katika pambano la ubingwa wa kuwania mkanda wa WBF.

Pambano hilo la Kimataifa lililopewa jina la 'The Return of Nakozi King', dhidi ya Abdumonem litafanyika Juni 10 mwaka huu katika ukumbi wa Diamond Jubilee, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, muandaaji wa pambano hilo, Siah Mosha alisema mapambano ya utangulizi yatakuwa manne kwa ajili ya kusindikiza pambano hilo. "Nawaomba Watanzania wajitokeze kwa wingi katika pambano hilo, kwani viingilio vya tiketi vitatangazwa hivi karibuni ili wadau na watanzania wajitokeze siku hiyo," alisema Siah.

Muandaaji huyo alitaja mapambano ya utangulizi kuwa Oscar Oscar atazichapa na Hassan Milanzi kutoka Zimbambwe, Juma Choki akichuana na Issa Nampepeche kwa ajili ya kuwania mikanda ya PST na Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC).

Wengine ni Stumai Muki akichapana na Chimwemwe Banda na Hasimi Maya atapigana na Mudochee Katembo kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### POGBA AWINDWA
BAYERN Munich wameingia kwenye kinyang'anyiro cha kumnunua mchezaji wa Manchester United, Paul Pogba, huku Juventus, Paris St-Germain, Real Madrid na Manchester City wakiwa tayari kuwinda saini ya kiungo huyo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 29. ***(Fichajes)***

### LEWIN ATAKIWA
KLABU ya Newcastle itawasilisha ombi la kumsajili mshambuliaji wa Everton na England, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 25. ***(Telegraph)***

### LEWANDOWSKI KUTOSAINI
ROBERT Lewandowski mwenye umri wa miaka 33 hatasaini mkataba mpya Bayern Munich, na mshambuliaji huyo wa Poland anaweza kuuzwa kwa Barcelona msimu huu wa joto. ***(Goal)***

### KOUNDE HUYO CHELSEA
CHELSEA wanataka kukamilisha usajili wa mlinzi wa Sevilla na Ufaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 23, mapema katika dirisha la joto. ***(Give me sport)***

### GUARDIOLA KUMALIZA
KOCHA Pep Guardiola atamaliza mkataba wake na Manchester City, ambao unamalizika mwaka 2023, badala ya kusaini nyongeza msimu huu wa joto. ***(Sky Sports, kupitia Manchester Evening News)***

### STERLING KUONDOKA
KIUNGO mshambuliaji wa Manchester City na England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 27, anatarajia kujiunga na moja ya klabu maarufu barani Ulaya iwapo ataondoka Etihad msimu wa joto, huku akitakiwa Arsenal na Tottenham. ***(The Athletic)***

### RICE KUSEPA
KLABU ya West Ham haitafanya mazungumzo zaidi na kiungo wa kati wa England, Declan Rice hadi dirisha la usajili la majira ya joto baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 kukataa mkataba wa miaka minane wenye thamani ya pauni milioni 83. ***(Sky Sports)***

### PHILLIPS KUNUNULIWA
ASTON Villa wanapanga kumnunua kiungo wa kati wa Leeds United na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 26. ***(Football Insider)***

### DE JONG AFUATILIWA
MANCHESTER United wanafuatilia hali ya kiungo wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong kule kwenye uwanja wa Nou Camp, lakini Barca wameweka bei ya pauni milioni 70 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Mail)***

### LUKAKU ANATAKA KUBAKI
MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28, anataka kubakia Chelsea msimu huu wa joto licha ya kuwa na wakati mgumu pale Stamford Bridge tangu kuhama kwake kutoka Inter Milan msimu uliopita wa joto. ***(Give me sport)***

### GOMEZ ASAKWA
MLINZI wa Liverpool na England, Joe Gomez mwenye umri wa miaka 24 anasakwa na kocha wa Aston Villa, Steven Gerrard msimu huu wa joto. ***(Mirror)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SALAH: MIMI FOWADI BORA DUNIANI

Asisitiza kwenye nafasi yake hakuna anamyefikia kwa ubora wake duniani kwa sasa na kwamba...

**LIVERPOOL, England**

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah amesisitiza kwamba, yeye ndiye mchezaji bora zaidi duniani katika nafasi yake.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri yuko mbioni kushinda Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu ya England, akijivunia mabao mengi kwenye ligi, huku akihusika moja kwa moja katika mabao 35 katika mechi 34 alizocheza.

Salah hivi karibuni alichaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa Mwaka wa Chama cha Waandishi wa Soka nchini Uingereza, na ana nafasi ya kuweka historia akiwa na Liverpool, kwani wameshinda Kombe la Carabao, na bado wanaliwinda taji la Ligi Kuu, Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Akizungumza na beIN SPORTS, Salah alisisitiza kwamba, hakuna mshambuliaji katika soka la dunia anayefikia kiwango chake.

"Ukinifananisha na mchezaji yeyote katika nafasi yangu, si kwenye timu yangu tu bali hata duniani, utagundua mimi ni bora," alisema.

"Siku zote mimi huzingatia kazi yangu na kufanya kwa ubora wangu, na namba zangu ni uthibitisho bora wa maneno yangu.

"Ninapenda kila wakati kupata changamoto mpya kwa ajili yangu, kufanya kazi kwa njia tofauti na kuleta mabadiliko, na hilo ni jukumu langu."

Kabla ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid - ambayo ni mechi ya marudiano kutoka fainali ya mwaka 2018, wakati Wahispania hao waliposhinda 3-1 - Salah ameiita kuwa ni "wakati wa kulipiza kisasi".

"Ndio - tulipopoteza katika fainali, ilikuwa siku ya huzuni kwetu sote," alisema. "Lakini, ndio, nadhani ni wakati wa kulipiza kisasi."

# Michezo

Jumamosi Mei 14, 2022

Nipashe






## Salah: Mimi fowadi bora duniani

# MWISHO WA MORRISON SIMBA SC?

●●●Klabu yatangaza kumpumzisha, mwenyewe ajibu asema kwa moyo mzito anatangaza kuwa nje kwa mechi zote zilizobaki ...




Morrison.

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imempa mapumziko hadi mwisho wa msimu huu mchezaji wake Bernard Morrison.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo kwenye mtandao wake rasmi wa Instagram imesema kuwa klabu imefikia maamuzi hayo baada ya pande zote mbili kukubaliana kwa lengo la kumpa nafasi kupumzika na kushughulikia mambo yake binafsi.

Aidha, klabu hiyo imemshukuru kwa mchango mkubwa kwa kipindi chote alichohudumu ndani ya timu hiyo.

"Tunatambua na kuthamini mchango wa Morrison katika miaka miwili aliyotumikia klabu yetu na kuisaidia kupata mafanikio kadhaa, ikiwemo kucheza robo fainali ya michuano ya Afrika mara mbili, kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ubingwa wa Kombe la FA, na Mapinduzi.

"Kwa mchango na mafanikio hayo, klabu inamshukuru mchezaji huyo kipenzi cha Wanasimba kwa kujitoa kwake kuipigania klabu yake," iliandika taarifa hiyo ambayo ilionyesha imetolewa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo ambaye ni Barbara Gonzalez.

Simba imemtakia kila la kheri winga huyo katika mapumziko yake na safari yake ya soka hapo baadaye.

Dakika chache baada ya taarifa hiyo, Morrison mwenyewe kupitia ukurasa wake wa facebook alisema: "Kwa Moyo mzito natangaza kwamba, nitakuwa nje ya uwanja kwa msimu uliobaki kutokana na matatizo ya kifamilia ambayo yako nje ya uwezo wangu na yanaweza kuathiri kiwango changu kwa timu kama nitaiwakilisha klabu. Mengi yanahitajika kusemwa kuhusu hilo, lakini naweza tu kuitakia kila la heri klabu katika mechi zetu zilizobaki. Nina matumaini na kusali ili mambo yangu yaishe haraka inavyowezekana ili ili niweze kujiunga tena na timu."

Morrison, mmoja kati ya wachezaji watukutu nchini ndani na nje ya uwanja, alisajiliwa na klabu hiyo msimu miwili iliyopita akitokea Yanga.

Hata hivyo usajili wake ulisababisha mvutano mkubwa kiasi cha Yanga kuamua kumpeleka kwenye Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji, akidaiwa kuwa alikuwa na mkataba wa klabu hiyo, huku mwenyewe akidai hakuwa nao, hivyo kusaini mkataba wa Simba.

Alishinda kesi hiyo mwaka 2020, lakini klabu ya Yanga haikukubali, ikaamua kulipeleka kwenye Mahakama ya Usuluhishi wa Kesi za Michezo Duniani (CAS), ambako kesi iliunguruma, huku akiwa anaitumikia klabu yake mpya, na akaibwaga tena.

Februari mwaka huu, alisimamishwa kwa utovu wa nidhamu kwa kile kilichodaiwa kutoroka kambini.

Pamoja na kuitumikia na kuipa mafanikio Simba na vituko vya hapa na pale, Morrison alishindwa kuitumikia timu hiyo mara mbili pale ilipotakiwa kwenda kucheza nchini Afrika Kusini na timu za Kaizer Chiefs na Orlando Pitates kwa nyakati tofauti kutokana na kuwa na matatizo na Idara ya Uhamiaji nchini humo.

## Simba kazi moja nusu fainali FA

**Na Adam Fungamwango**

IWAPO Simba itashinda leo kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Pamba, itakutana na watani wake wa jadi Yanga kwenye mechi ya nusu fainali, kusaka bingwa atakayeiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka barani Afrika.

Mechi hiyo itachezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ambapo Simba itakuwa na kazi moja tu kupata ushindi ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kutetea tena kombe hilo kwa mara ya tatu mfululizo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amesema maandalizi yamekamilika na kinachosubiriwa ni kuingiza timu uwanjani.

"Tumejiandaa na mchezo huu mgumu, kucheza na timu ambayo haina cha kupoteza ni hatari kubwa. Pamba kufika hatua ya robo fainali kwake ni mafanikio makubwa, ukicheza na timu iliyoridhika ni hatari sana, tutaingia kwa tahadhari na kwa kuiheshimu kwa sababu mpira una maajabu yake na Simba tumeshawahi kupitia maajabu hayo," alisema Ahmed.

Simba ilishawahi kutolewa kwenye kombe hilo kwa nyakati tofauti dhidi ya timu za Mashujaa FC ya Kigoma na Green Warriors ya Dar es Salaam.

"Lakini kwa sisi Simba ni jukumu letu kuhakikisha tunapata ushindi kwenye mechi hii kwa kuishikisha adabu Pamba ili tuweze kuingia hatua ya nusu fainali, hakuna mtu atakayetuelewa duniani hapa kama tukitolewa na Pamba," alisema Ahmed.

Katibu Mkuu wa Pamba, Johnson James amekiri mechi itakuwa ngumu kutokana na ubora ambao Simba imekuwa ikiuonesha kwenye mechi za hivi karibuni, lakini hawaiogopi.

"Hatuwezi kuiogopa Simba kwa sababu tumeingia hapa kwa uwezo wetu, hata kufika hatua hii tumeifunga Dodoma Jiji, timu ya Ligi Kuu kama ilivyo Simba. Hatukupata nafasi hii kwa bahati mbaya tuna timu bora, mwanzo kilichotusumbua ni hali ya hewa, lakini kwa sasa tumekaa wiki nzima hapa tangu tucheze mechi ya Championship, kwa hiyo haitotusumbua tena," alisema Katibu Mkuu huyo.

Pamba ipo Dar es Salaam tangu Mei 8, ilipocheza mechi ya Championship dhidi ya DTB na kufungwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Uhuru, mechi ambayo iliwapandisha Ligi Kuu wapinzani wao hao.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >